# Nipashe

Jumanne Septemba 8, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580332

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Ilani NCCR yajinadi 50/50 kwenye vyombo vya uwakilishi

UKURASA 3




UKURASA 11

# Ni ahadi zaidi

• **JPM** kuifanya Mwanza kitovu cha biashara, Lissu aahidi neema Zanzibar, Lipumba aja na uwekezaji mkubwa Kusini... *Uk. 2*



Mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, akihutubia maelfu ya wananchi katika mkutano wake wa hadhara wa kampeni za uchaguzi mkuu katika uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**

## Adaiwa kuchoma moto basi kuepa deni

UKURASA 4



Mgombea urais kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akihutubia wakati wa ufunguzi wa kampeni za urais kwa chama hicho, katika viwanja vya Sabasaba, mjini Mtwara jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwasili katika viwanja vya Kibandamaiti, Unguja jana, kwa ajili ya kuhutubia katika mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store


# Kubenea kufikishwa kortini tuhuma utakatishaji fedha

UKURASA 3


Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

# JPM kuigeuza Mwanza kitovu cha biashara

**Na Gwamaka Alipipi,** MWANZA

MGOMBEA urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amesema atahakikisha Jiji la Mwanza linakuwa kitovu cha biashara kwa nchi za Maziwa Makuu.

Amesema tangu alipoingia madarakani mwaka 2015, alijikita kuimarisha miundombinu ya usafiri, huduma za kijamii zikiwamo maji, elimu, afya na umeme katika jiji hilo.

Aliyasema hayo jana katika uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa, wakati akiwahutubia maelfu ya wananchi waliojitokeza kumsikiliza akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dk. Magufuli alisema katika kuhakikisha Jiji la Mwanza linakuwa kitovu cha biashara, upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza umefanyika kwa kilometa 3.5, ili kuziwezesha ndege kubwa kutua.

"Katika mipango ya miaka mitano ijayo kama nitachaguliwa tutanunua ndege zingine tano, ambazo zingine zitakuwa zinatoka Mwanza kwenda moja kwa moja Ulaya."

"...Ukipanda hapa unakwenda moja kwa moja Jiji la London, Uingereza, ukitoka London unateremka Mwanza. Hiyo ndiyo dhamira yetu tuliyoipanga."

Dk. Magufuli alisema katika kutimiza hilo, mkakati uliopo ni kuhakikisha meli za MV Mwanza na Victoria zinaanza kufanya safari kutoka Mwanza-Kemondo-Uganda-Kisumu-Musoma, kisha zirudi Mwanza, lengo ni kuwawezesha wananchi wa Mwanza kutengeneza pesa pamoja na kupanua biashara.

Pia ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Isaka hadi Mwanza utapanua fursa za kibiashara kwa wananchi wa jiji hilo pamoja na kukuza kipato.

Akielezea mafanikio yaliyopatikana katika Jiji la Mwanza katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake, alisema ujenzi wa barabara kutoka Nyakato-Veta-Buswelu, Makongoro-Mwaroni, ujenzi wa Daraja la Furahisha pamoja na stendi ya Nyegezi.

Kwenye usafiri wa majini, Dk. Magufuli alisema serikali imekarabati chelezo, ukarabati na ununuzi wa meli mpya, pamoja na ukarabati vivuko vya Mv Mara na Ilemela.

Kwenye sekta ya anga, Dk. Magufuli alisema, serikali imenunua rada kubwa, ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege Mwanza pamoja na eneo la kuhifadhia minofu ya samaki.

Kwenye sekta ya afya, Dk. Magufuli alisema serikali imeboresha huduma za kibingwa katika Hospitali ya Rufani ya Sekou-Toure, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa saratani, pamoja na ujenzi wa miundombinu katika afya kwa gharama ya Sh. bilioni 11.4.

Kuhusu elimu, Dk. Magufuli alisema serikali imejenga nyumba za walimu, madarasa, mabweni ya wanafunzi, ukarabati wa shule kongwe, pamoja na kutoa Sh. bilioni 53.7 kufanikisha huduma ya elimu bure mkoani Mwanza.

Kwenye maji, Dk. Magufuli alisema zaidi ya Sh. bilioni 92 zimetumika kufanikisha miradi ya maji Nansio, Magu na Misungwi. Alisema vijiji 144 vimeshafikiwa na huduma ya umeme, huku Sh. bilioni 30 zikiwa zimetengwa kwa ajili ya kumalizia vijiji vilivyosalia.

Sekta ya madini, alisema serikali imetoa leseni 147 kwa wachimbaji wadogo, ujenzi wa kiwanda cha kusafishia madini chenye uwezo wa kusafisha kilo 300 kwa siku.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano kupitia sheria mpya ya madini na kulinda rasilimali ilipitishwa pamoja na kufikia makubaliano na kampuni ya uchimbaji madini ya Barrick ya kuanzisha kampuni mpya ya Twiga.

Katika kampuni hiyo, Barrick wanamiliki asilimia 84 na Tanzania 16, na faida itakayopatikana itagawanywa asilimia 50 kwa 50.

Alisema makao makuu ya Kampuni ya Twiga yatakuwa Mwanza. Faida itakayopatikana Tanzania itapewa Dola za Marekani zaidi ya milioni 100. (Sh. bilioni 230).

Mgawanyo wa fedha hizo ni kwamba Dola milioni tano (Sh. bilioni 11.5) zitatolewa kama mchango wa utafiti, uwekezaji na kuanzisha uwekezaji wa kuchenjua madini.

Alisema Dola milioni 10 zitatolewa kama mchango wa kuimarisha uwezo wa mitambo ya serikali kupima viwango vya madini yaliyozalishwa.

Pia alisema Dola milioni tano zitatolewa kama mchango wa uwezo wa kuhifadhi madini katika migodi. Dola milioni 10 katika kipindi cha miaka 10 zitatolewa katika vyuo vikuu kuendeleza na kuimarisha mafunzo ya wataalamu wa madini na wahandisi wa madini na Dola milioni 40 zitatolewa kuboresha barabara za lami jijini Mwanza pamoja na kujenga makazi ya wafanyakazi wa migodini katika jiji hilo.

Alisema Dola milioni sita katika kila mwaka kwenye kila kilo moja ya dhahabu itakayouzwa kupitia makinikia zitawekwa katika mfuko wa maendeleo kwa manufaa ya jamii zinazozunguka migodi.



Mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wananchi katika mkutano wa kampeni Kijiji cha Kibiti, mkoani Pwani jana. **PICHA: OMR**

# Lipumba aahidi uwekezaji mkubwa mikoa ya Kusini

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), jana kilizindua kampeni zake za uchaguzi mkoani Mtwara, huku mgombea wake wa urais, Prof. Ibrahim Lipumba, akiahidi kwamba akichaguliwa, atahakikisha anainua uchumi katika mikoa ya Kusini.

Alisema atafanya hivyo kwa kukaribisha wawekezaji wa ndani na nje katika fursa zote zilizopo katika mikoa hiyo ikiwamo gesi.

Alisema serikali yake itaimarisha uchumi kwa kuhakikisha kila mwaka unaongezeka kwa asilimia 10 na kuongeza ajira kwa vijana.

Jambo jingine ambalo alisema serikali yake itafanya ni kuipatia nchi Katiba mpya yenye misingi mizuri itakayojenga umoja wa kitaifa na itakayolinda demokrasia na haki za binadamu.

Pia alisema serikali yake itahakikisha inajenga muungano wenye tija badala ya wenye matatizo.

Jambo lingine alisema ataboresha sekta ya elimu kwa kuhakikisha kila shule inakuwa na kompyuta kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanafunzi kuhimili ushindani wa dunia na kujifunza kugha mbalimbali.

Kadhalika, aliahidi kuinua sekta ya kilimo kwa kuhakikisha wakulima wanapata zana za kisasa.

"Kanda ya Kusini imajaliwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwamo korosho, kahawa, pamba, katani chai, tumbaku na gesi, lakini hainufaiki na rasiliamali hizi, mkinichagua kuwa rais nitahakikisha ninainua uchumi wa mikoa hii kupitia fursa zilizopo," alisema Prof. Lipumba.

"Mna bahati, lakini uvuvi unaofanyika mikoa ya Kusini ni duni na usiotumia vyombo vya kisasa, wavuvi hawajapewa wa kutumia uwezo wa kuitumia bahari katika sekta ya uvuvi. Kuna fursa kubwa za kutumia ufukwe katika utalii, nichagueni ili nifufue haya yote."

Profesa Lipumba pia aliahidi kwamba kama atachaguliwa, ataboresha sekta ya afya kwa kuhakikisha wanawake na watoto wanapata huduma bora.

# Lissu aahidi haki Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia CHADEMA, Tundu Lissu, aliahidi endapo atapata urais atahakikisha anairejesha haki ya Wazanzibari kwa wale wote waliodhulumiwa.

Alitoa ahadi hiyo jana alipokuwa akihutubia mkutano wa kampeni katika viwanja vya Demokrasia Kibandamaiti, ambapo alisema kuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ndiye anayeweza kuking'oa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alidai kuwa maamuzi makubwa ya kisiasa kuhusu Zanzibar hufanyika Tanzania Bara. Alisema kuwa uchaguzi wa mwaka huu wapinzani wana uwezo wa kuishinda, lakini ni lazima wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara wakafanya uamuzi mgumu.

Alisema kuna haja kwa vyama vingine vya siasa kumuunga mkono Maalim Seif, ambaye ana uwezo wa kuishinda CCM. Alisema maslahi ya Wazanzibari katika uchaguzi wa mwaka huu ni kumuunga mkono Maalim Seif.

Alisema kumuunga mkono mgombea huyo wa ACT haina maana kuwa wanawasaliti wagombea wao.

Alisema kwa upande wa urais wa Tanzania, CHADEMA ina uwezo wa kushinda, hivyo vyama vingine havinabudi kuiunga mkono. Anayeiweza kuishinda CCM ni CHADEMA hivyo ni vyema kukiunga mkono. Kadhalika, Lissu alieleza kuwa lazima yafikiwe maridhiano ya kitaifa ili kusameheana na kuunda kwa tume huru ya katiba.

Aidha, alisema watapigania haki ili Taifa liinuke na hawatakuwa tayari kuibiwa kura katika uchaguzi wa Oktoba. Naye mgombea mwenza wa CHADEMA, Salum Mwalimu Juma, alisema kuwa watakaposhinda atahakikisha anamshauri Rais kuwatoa mahabusu viongozi wa Jumuiya ya Uamsho.

Aidha, Mwalimu alisema mambo muhimu watakayoyafanyia kazi watakapoingia madarakani ni kupatia mamlaka kamili Zanzibar, kulipa fidia mauaji ya Wazanzibari yaliotokea Pemba mwaka 2001.

# Kubenea kortini tuhuma utakatishaji fedha

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA Mbunge wa Ubungo, Saed Kubenea, anatarajiwa kufikishwa mahakamani kwa tuhuma za kuingiza nchini fedha za kigeni kinyume cha kanuni, taratibu na sheria za nchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mashataka (DPP), Biswalo Mganga, Kubenea alikamatwa na Jeshi la Polisi Septemba 5, mwaka huu, akiwa katika gari la abiria lenye namba ya usajili T. 645 DKR akitokea katika mpaka wa Tanzania na Kenya, eneo la Namanga akielekea Arusha mjini.

Kwa mujibu wa Mganga, baada ya kumkamata walimpekua mtuhumiwa huyo na kukutwa na vitu mbalimbali zikiwamo Dola za Marekani 8,000 (sawa na Sh. milioni 18.6), Shilingi 491,700 za Kenya (sawa na Sh. milioni 10.5) na Sh. 71,000.

Pia alikutwa na tiketi ya basi la Super Couch, lenye namba ya usajili KCP. 4230 ya Septemba 5, mwaka huu kutoka Nairobi, Kenya kwenda Namanga, mkataba wa makubaliano (Memorandum of Understanding) kati ya Hali-Halisi ya Tanzania na Buni Media Limited ya Kenya.

Vingine ni risiti ya malipo ya hoteli After 40 Hotels Limited, iliyopo Nairobi nchini Kenya yenye jina la Kubenea Saed Ahmed, kama mgeni kuanzia Septemba 3 hadi 5, mwaka huu pamoja na pasi yake ya kusafiria.

Kwa mujibu wa Mganga, baada ya kukamatwa, mtuhumiwa alieleza kuwa alifika mkoani Arusha Septemba 2, mwaka huu, akitokea Dar es Salaam na kufikia katika hoteli iliyopo Arusha mjini na kwamba Septemba 3, mwaka huu, alikwenda kulala kwa kaka yake, na Septemba 4 alikwenda Namanga na kupokea fedha taslimu tajwa hapo juu kutoka kwa raia wa Kenya.

"Baada ya kupitia ushahidi uliokusanywa, nimebaini kuwa mtuhumiwa hakufikia katika hoteli aliyoitaja Arusha mjini, wala kulala kwa kaka yake kama alivyoeleza. Mtuhumiwa tajwa alivuka mpaka usio rasmi na kuelekea Nairobi nchini Kenya na kisha kurejea nchini Tanzania bila kutumia mpaka rasmi mnamo Septemba 5 mwaka huu," ilieleza taarifa hiyo ya DPP.

"Mtuhumiwa tajwa aliingiza nchini fedha za kigeni bila kutoa tamko rasmi la kisheria kinyume na masharti ya Kanuni za the Anti-Money Laundering (Cross-Border Declaration of Currency and Bearer Negotiable Instruments) Regulations, 2016 zikisomwa pamoja na kifungu cha 28B(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia Utakasishaji wa Fedha Haramu Na. 12 ya Mwaka 2006."

DPP alisema baada ya jana kujiridhisha na uwapo wa ushahidi wa kutosha dhidi ya Kubenea, na misingi ya kikatiba inayomwongoza kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 59B(4)(a) hadi (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, aliidhinisha mashtaka dhidi ya mbunge huyo wa zamani.

Mganga alisema makosa ambayo ameyainidhinisha kwa Kubenea ni la kuingia nchini Tanzania kinyume cha Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 marejeo ya mwaka 2016, na la pili ni la kuingiza nchini fedha za kigeni bila kutoa tamko kinyume cha kanuni za utoaji tamko la fedha mpakani za mwaka 2016.

## Mgombea urais ADA-TADEA arejesha fomu akiipa tano ZEC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, jana amerejesha fomu Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ili aweze kuteuliwa kuwa mgombea na kwamba ana imani na Tume hiyo.

Khatib anakuwa mgombea wa pili kurejesha fomu hiyo baada ya mgombea wa CCM, Dk. Hussein Mwinyi. Mgombea huyo wa TADEA alichukua fomu Agosti 27, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi za ZEC baada ya kurejesha fomu, Khatib aliwataka wagombea wenzake ambao watapitishwa na Tume kushindana kwa hoja, sera, kuhubiri amani na kuweka uzalendo mbele ya nchi wakati wanapokuwa katika majukwaa ya kisiasa. Alisema huu si wakati wa kuhubiri siasa za chuki na uhasama na badala yake viongozi wa vyama vya siasa wahubiri amani ya nchi ili uchaguzi umalize kwa amani bila ya damu kumwagika.

Alisema kuwa lengo la chama chake ni kushinda katika uchaguzi mkuu na kuwa Rais wa Zanzibar, lakini endapo kura hazitotosha ataheshimu uamuzi wa Tume. Alisema chama hicho kitafanya kampeni zenye kulenga umoja, mshikamano na utulivu ili kunadi sera zao ikiwamo usawa wa jamii.

Vile vile, alisema uchaguzi usiwe sababu ya Wazanzibari kulumbana au kufarakana hivyo ni vyema kuwa wamoja kabla na baada ya uchaguzi ili nchi iweze kupata maendeleo na kumuunga mkono Rais atakayeshinda katika uchaguzi huo.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib (kulia), akirejesha fomu za kuomba uteuzi wa nafasi hiyo, kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud katika ofisi za tume hiyo, eneo la Maisara, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ilani ya NCCR yajinadi 50/50 kwenye vyombo vya uwakilishi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimesema kikifanikiwa kuingia madarakani kitahakikisha kunakuwa na idadi sawa ya wanaume na wanawake katika vyombo vya uwakilishi na kupanua mfumo wa uwakilishi wa uwiano wa 50 kwa 50.

Hayo ni miongoni mwa vipaumbele 10 vilivyomo katika ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020 ya chama hicho.

Ilani ya chama hicho inaeleza kwamba itaweka sheria ambayo mwanamke atakuwa miongoni mwa viongozi wakuu wa serikali husussani katika nafasi za urais, makamu wa rais na waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano.

Nafasi nyingine ya mwanamke katika ilani ya chama hicho ni katika nafasi ya spika wa bunge.

Pia inaeleza namna itakavyozingatia usawa wa kijinsia katika nafasi mbalimbali za kiutawala ikiwamo mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya, mabalozi, makatibu wakuu wa wizara, makamishna, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, wenyeviti wa wajumbe wa bodi za mashirika ya umma.

Ilani hiyo inaeleza kwamba itahakikisha pia katika sekta na taasisi za umma na binafsi zinadumisha dhana ya usawa huo wa kijinsia.

Katika sekta ya elimu, ilani ya NCCR-Mageuzi inaeleza kupunguza miaka ya elimu ya sekondari kutoka minne ya sasa ya kidato cha kwanza mpaka cha nne hadi kufikia miaka miwili ambayo itatolewa bure.

Mbali na hilo, pia inaeleza kwamba itaweka mpango wa wasichana wote wa elimu ya msingi wanaopata ujauzito kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Itapanua elimu ya vyuo vikuu kwa kuanzisha vyuo vikuu vipya ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa muda mrefu wa kuupatia kila mkoa angalau chuo kikuu kimoja pamoja na kubadili sera ya elimu ya taifa kwa kuipa maudhui, na upeo kulingana na mahitaji ya kimaadili ya kimaendeleo ya taifa.

Inaeleza kwamba kitaanzisha utaratibu wa shule za bweni za wasichana, ili kuzuia mimba za utotoni, kuepuka kutembea umbali mrefu na kuondokana na kufanya shughuli za nyumbani ambazo zimekuwa zikiathiri vibaya maendeleo yao ya kitaaluma.

NCCR-Mageuzi katika ilani yake kadhalika, inaeleza itaanzisha chuo cha taifa cha kufundisha watu wazima hasa viongozi kutoka sekta mbalimbali ili kujenga utamaduni wa viongozi wenye kupenda kujielimisha.

**VYOMBO VYA HABARI**

Kwa upande wa vyombo vya habari, NCCR-Mageuzi kinasema kitalinda haki na uhuru wa vyombo vya habari kama ilivyoainishwa katika mikataba ambayo nchi ilitia saini au kuridhia.

Inaeleza ili kuviwezesha vyombo vya habari na asasi zisizo za kiserikali kuwa huru na kufanya kazi vizuri kwa manufaa ya wananchi, serikali itakayoongozwa na NCCR-Mageuzi itahakikisha sekta ya habari inatambulika katika Katiba mpya.

DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUFANYA **MRADI WA MAJI KIBONDO NA KUKARABATI MAJENGO**

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI WENYE NIA KULETA ZABUNI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA **TAREHE 07.09.2020 HADI TAREHE 28.09.2020** KWA AJILI YA MRADI WA MAJI KIBONDO NA TAREHE 08.09.2020 HADI **TAREHE 21.09.2020** KWA AJILI YA UKARABATI MAJENGO SIKU ZA KAZI **SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI.** TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255627 428 470 au barua pepe jackson.maseke@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA KWA AJILI YA UKARABATI WA MAJENGO TAREHE 23.09.2020** NA 29.09.2020 ZABUNI ZITAFUNGULIWA ZA MRADI WA MAJI SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI KIBONDO VINGINEVYO NI BATILI.**

115890202

# Mbaroni tuhuma kuchoma basi kisa kukwepa deni

**Na Frank kaundula,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linawashikilia watu watatu akiwamo mmiliki wa basi la kampuni ya HBS lenye namba za usajili T 321 DKW, Ahmedi Hemed (25) kwa tuhuma za kuchoma moto basi hilo na kusingizia kuwa limewaka moto baada ya kushindwa kufunga breki.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema watuhumiwa hao walikula njama ya kufanya tukio hilo baada ya mmiliki kushindwa kulipa deni la basi hilo linalodaiwa kufikia zaidi ya Sh. milioni 200 na moja ya taasisi ya kifedha nchini.

Kamanda Mutafungwa alisema kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 27, mwaka huu majira ya saa nane usiku katika eneo la Wami Luhindo, Barabara ya Morogoro-Dodoma, wakati dereva wa gari hilo, Riziki Abraham, alisema chanzo cha ajali ni tatizo lililotokea katika mfumo wa breki.

Alisema kuwa baada ya uchunguzi wa kina mmiliki wa gari hilo alikiri kufanya tukio hilo kwa kulichoma kwa lengo la kukwepa kulipa deni analodaiwa.

"Baada ya kumuhoji kwa mara ya pili alikiri kupanga njama hiyo kwa kulimwagia mafuta ya thinner na petrol, kisha kuliwasha moto ili bima ilipe taasisi hiyo ya kifedha kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 200 zinazodaiwa," alisema Mutafungwa.

Alisema, baada ya kubaini upungufu huo waliwataka wahusika kufika kituo cha polisi kwa mahojiano ndipo watuhumiwa hao wakaamua kulitorosha gari hilo na kutaka kulipeleka jijini Dar es Salaam.

Alisema walipojaribu kuwafuatilia walifanikiwa kukamata gari hilo katika moja ya kituo cha mafuta nje kidogo ya mji wa Morogoro likiwa limepakiwa katika lori lenye namba za usajili T336 DDX lililokuwa likiendeshwa na Sadam Seif, mkazi wa Morogoro.

"Askari wa Zimamoto kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walizima moto huo na kufanya uchunguzi wa awali na kubaini kuwa basi hilo halikuwa na injini, difu, usukani wala viti vya kukalia abiria ndipo uchunguzi wetu ukaanzia hapo mpaka tumewakamata," alisema Mutafungwa.



Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji mstaafu Juxon Mlay (katikati), akimwapisha mpigapicha za habari mwandamizi, Khalfan Said kuwa jaji wa tuzo za EJAT, kushoto ni Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaji wa Tuzo za EJAT waapishwa

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limeapisha jopo la majaji sita watakaopitia na kuchagua kazi zilizo bora kutambuliwa kati ya kazi 450 zilizowasilishwa kushindanishwa katika makundi 21 ya Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari wa Tanzania (EJAT) mwaka 2019.

Katibu Mtendaji wa MCT na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi EJAT, Kajubi Mukajanga, alitangaza jopo hilo la majaji, wakiongozwa na mwenyekiti wao, Pudenciana Temba, jana jijini Dar es Salaam.

Aliwataja majaji wengine kuwa ni Pili Mtambalike, Imane Duwe, Mohammed Kissengo, Mkumbwa Ally na Khalfan Said, ambao waliapishwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya MCT, Jaji mstaafu, Juxon Mlay.

Mukajanga alisema kati ya makundi 21 yanayoshindaniwa katika tuzo hizo, matatu ni mapya ambayo ni Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu, Hedhi Salama na Athari ya Kemikali kwa Afya ya Mazingira.

Alisema kati ya kazi 450 zilizowasilishwa, waandishi wa Dar es Salaam, wameongoza kuwasilisha kazi 154, wakifuatiwa na mkoa wa Mwanza kazi 30, Zanzibar na Kagera wakiwa na nafasi ya tatu kwa kuwasilisha kazi 29 kila mmoja.

Aliitaja mikoa mingine kuwa ni Tanga ya nne iliyowasilisha kazi 28 na Arusha ni ya tano kwa kazi 21 na zote zimetoka katika vyombo vya habari 68.

Mukajanga alibainisha kuwa, vyombo vya habari vya kielektroniki viliwasilisha kazi 215 ambazo ni sawa na asilimia 53.3 ya kazi zote, magazeti kazi 180 sawa na asilimia 44.7 na vyombo vya mtandaoni kazi nane sawa na asilimia mbili.

"Kampuni ya Mwananchi Communications Limited imewasilisha idadi ya kazi 61, ikifuatiwa na The Guardian Limited 41, Tanzania Standard Newspapers 33, Pangani FM 25 na TBC 24," alisema Mukajanga.

Alisema tuzo hizo kwa mara ya kwanza tangu zianze kutolewa nchini mwaka 2009, sherehe zake zitafanyika nje ya jiji la Dar es Salaam katika Jiji la Tanga, Septemba 28, mwaka huu.

Mukajanga alitaja sababu ya kucheleWa kutolewa kwa tuzo hizo za mwaka jana ni kutokana na kuwapo kwa ugonjwa unaosababishwa homa ya mapafu wa COVID-19.

Aidha, alisema tukio hilo litaenda sambamba na uzinduzi wa tuzo za EJAT kwa mwaka 2020.

Alisema siku hiyo pia utafanyika Mkutano Mkuu wa (NGC) wa MCT na washiriki ni wanachama wa baraza pamoja na vyombo vya habari , klabu za waandishi na vyuo vya uandishi wa habari nchi nzima.

# Mwalimu kortini madai kumhonga RAS 90,000/-

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Tabora, imemfikisha mahakamani, mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kizengi, Kondwani Peter Masata, kwa tuhuma za kutoa rushwa kinyume cha kifungu cha 15 (1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora, Musa Chaulo, ilieleza kuwa mwalimu huyo angefikishwa mahakamani kwa kosa la kutoa rushwa ya Sh. 90,000 kama kishawishi kwa Katibu Tawala Mkoa huo ili amhamishie Manispaa ya Tabora.

Chaulo alisema kuwa, uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU ulibaini kuwa, mtuhumiwa huyo, aliomba uhamisho na kwa nyakati tofauti alikuwa akishawishi kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS) na baadaye kutoa kiasi hicho cha fedha kwa njia ya simu ili kuhamishwa Manispaa ya Tabora toka Kizengi.

Katika tukio lingine, TAKUKURU kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ilimfikisha mahakamani, Mhasibu wa Chuo cha Ualimu Tabora, Fidelis Myovella na mfanyabiashara wa Manispaa ya Tabora, Joseph Kaizerege kwa kosa la kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri.

Alisema kosa hilo ni kinyume cha kifungu cha 22 na 32 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namna 11 ya mwaka 2007 ikisomwa pamoja na Aya ya 21 Jedwali la kwanza na kifungu cha 57(1) na 60 (2) ya Sheria ya Uhujumu Uchumi (sura 200 marejeo ya mwaka 2002).

Chaulo alisema Fideli Myovella akiwa mwajiriwa serikalini alitumia nyaraka ya kuombea vifaa yenye maelezo ya uongo kuonyesha kuwa kampuni ya KANIJA & SONS Enterprises wana haki ya kulipwa Sh. milioni 12.2 kama malipo ya kusambaza vifaa vya umeme kwa ajili ya ukarabati wa chuo hicho ilhali siyo kweli.

Alisema Joseph Kaizerege kwa lengo la kumdanganya mwajiri wake ambaye ni mkuu wa chuo hicho, alitoa hati ya madai yenye maelezo ya uongo kuonyesha kuwa wanadai kiasi hicho cha fedha.

"Ninawashukuru wananchi wa mkoa wa Tabora kwa ushirikiano mnaoutoa kwa TAKUKURU na inawaasa watumishi na wananchi wa mkoa huu, kutojihusisha na vitendo hivyo kwa sababu tutawafikisha kwenye vyombo vya sheria wale wote wasiyo waadilifu," alisema Chaulo.

Aidha, aliwataka Watanzania kutowakubali wagombea wanaowarubuni kwa rushwa na badala yake watoe taarifa za vitendo hivyo kupitia APP au namba 113 (bure) au kufika ofisi zao zilizopo wilaya zote nchini.

# PM: Zipo fedha za kutosha kuboresha huduma za jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ina fedha za kutosha kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania katika kuboresha huduma za jamii zikiwamo za afya, maji na elimu.

Ameyasema hayo jana alipohutubia mkutano wa kampeni katika uwanja wa soko la Holili Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, wakati akimwombea kura Rais John Magufuli na mgombea ubunge wa Jimbo la Rombo, Prof. Adolf Mkenda na wagombea udiwani kupitia CCM.

Majaliwa aliwataka wananchi wasifanye mzaha siku ya kupiga kura itakapofika, wasimchague mtu kwa sababu ya ushabiki, badala yake wamchague Rais Magufuli na wagombea wote wa CCM, ili waweze kushirikiana katika kuendeleza miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Tunaomba kura zenu wanaHolili na Watanzania wote kwa Rais Magufuli ili akaendelee kuboresha maendeleo katika sekta ya elimu itakayotuwezesha kuwa na wataalamu wengi. Nawaomba mumchague kwa sababu ameitendea haki nchi yetu na ni kiongozi mcha Mungu na mpenda maendeleo."

Akizungumzia kuhusu changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama inayowakabili wakazi wa Holili, Majaliwa alisema tayari serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina kuona namna watakavyoyatoa maji kutoka Ziwa Chala na kuyasambaza kwa wananchi.

Alisema mradi mwingine wa maji unaotekelezwa katika wilaya hiyo ni wa maji Njoro II (Tarakea). "Serikali imekamilisha mradi huu kwa shilingi milioni 200 na unatoa huduma ya maji katika eneo la Tarakea. Malengo ya serikali kwa sasa ni kutafuta fedha ili kuupanua mradi huo na kuweza kutoa maji katika maeneo mengine ya Tarafa nzima ya Tarakea," alisema.

Kwa mujibu wa Majaliwa, mradi wa kijiji cha Ngareni wenye thamani ya Sh. milioni 812.4 uliohusisha ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji la lita 75,000 na ujenzi wa vituo 15 vya kuchota maji pamoja na ufungaji wa bomba za njia kuu na njia za kusambaza maji umekamilika.

Alisema katika kuhakikisha huduma ya maji na salama inawafikia wakazi wote wa Wilaya ya Rombo kikamilifu, Julai mwaka huu serikali ilivunja Kampuni ya Maji ya Kill Water na kuanzisha Mamlaka ya Maji (ROWASA).

## Mgombea Bukoba amwaga ahadi lukuki

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MGOMBE ubunge wa Jimbo la Bukoba Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Stephen Byabato, amewaomba wakazi wa jimbo hilo kumchagua kuwa mbunge wao, ili kuwapunguzia kero zinazowakabili.

Miongoni mwa kero hizo zinahusu ardhi, hasa wanawake na watu wenye kipato cha chini, ambao wamekuwa wakinyanyaswa kutokana na hali duni ya kiuchumi.

Akizungumza katika uwanja wa Uhuru wakati wa kuzindua rasmi kampeni za CCM Jimbo la Bukoba Mjini, Byabato ambaye ni wakili wa kujitegemea alisema endapo atachaguliwa atashirikiana na mawakili wenzake kupunguza migogoro ya ardhi na kuhakikisha watu wanapata haki zao. Kwa upande wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimepanga kuzindua rasmi kampeni za mgombea ubunge wa chama hicho katika Jimbo la Bukoba Mjini, Chief Kalumuna, Septemba 19 katika uwanja wa Uhuru ulioko katika Manispaa ya Bukoba.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Bukoba, Victor Sherejey, alisema wamechelewa kuzindua kutokana na kushughulikia mapingamizi yaliyowekwa dhidi ya wagombea udiwani katika kata tatu na kusubiri sera na ilani ya chama.

Sherejey alisema kuwa katika Jimbo la Bukoba Mjini waliwekewa mapingamizi madiwani wa tatu wa kata za Kibeta, Kahororo na Kagondo na kuwa katika kata moja ya Kibeta walishinda pingamizi na katika kata za Kahororo na Kagondo wagombea wao waliondolewa.

"Hatukuridhika na hatua ya madiwani wetu wawili kuondolewa, tumekata rufani tume ya taifa na sasa tunasubiri maamuzi ya tume," alisema.



Ujenzi wa barabara za juu (Ubungo Interchange) katika makutano ya Barabara za Mandela, Morogoro na Sam Nujoma eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam, ukiendelea kwa kasi. Mradi huo, unatarajiwa kuondoa adha ya msongamano mkubwa wa magari katika makutano hayo, pindi utakapokamilika. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Matiko akemea kejeli, matusi

**Na Timothy Itembe,** MARA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Tarime Mjini, Esther Matiko wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ametaja baadhi ya kasumba zinazokwamisha wanawake kujitokeza kugombea nyadhifa za uongozi kuwa ni kejeli na matusi kwa wanawake.

Alisema hayo jana wakati akizindua mkutano wa kampeni za uchaguzi uliofanyika viwanja vya Serengeti maarufu Shamba la Bibi, ambao ulihudhuriwa na wagombea wengine wa chama hicho akiwamo Esther Bulaya, kutoka Bunda Mjini, Catherine Ruge, Jimbo la Serengeti, Julius Mtatiro wa Musoma Mjini na John Heche, Jimbo la Tarime Vijijini.

"Tunahitaji kuwa na kiongozi wa maono ya maendeleo ambaye anashirikiana na wananchi wake kuibua miradi hata kama ni mwanamke au mwanaume haijalishi, wala hatuhitaji kusikiliza kejeli zinazotolewa juu yangu na baadhi ya watu ambao wengine ni viongozi ambao wakitoa matusi tena hadharani," alisema Matiko.

Alisema miaka yake mitano amefanya maendeleo mengi ndani ya jimbo lake kwa kuzingatia, kipaumbele cha elimu bora, afya bora, miundombinu pia michezo haikubaki nyuma.

Aliwashukuru wananchi kwa kumwamini na kumpa kura za kutosha zilizomwezesha kuingia bungeni na kuwaomba tena kumwamini na kumpa kura za kutosha zitakazomwezesha kuingia bungeni na kuwaletea maendeleo na atahakikisha maslahi ya wafanyakazi yana boreshwa, wafanyabiashara pamoja na wakulima

Kwa upande wake Catherine, ambaye anagombea Jimbo la Serengeti, alisema mila kandamizi zinazoambatana na matusi na kejeli kwa kinamama zinapaswa kukemewa na kukomeshwa na jamii kipindi hiki cha sayansi na teknolojia.

Alisema matusi na kejeli kwa wagombea wanawake ni moja ya kikwazo kwa wanawake kinachowakwamisha kujitokeza kugombea nyadhifa mbalimbali za uongozi.

Alisema ukatili wa kijinsia ambao unaendekezwa na baadhi ya makabila nchini haupaswi kuwapo, bali kukemewa na jamii kwa kuzingatia kuwa nchi nyingi zimesaini mikataba ya kimataifa ya kupinga ukatili Tanzania ikiwamo.

Aliitaka pia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutenda haki ya kutangaza mgombea yeyote ambaye atakuwa ameaminiwa na wananchi kwa kumpa kura nyingi za kutosha kutangazwa kuwa mshindi katika eneo ambalo ameomba kuwatumikia.

**JAHMUHRI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE
ILIYOPO TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NO. 13/2020**

**EMMA MWENDA**

**Dhidi ya**

**OMARY SALEHE**

**Kwa: OMARY SALEHE
DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa tarehe 10/9/2020 saa 8:30 Asubuhi, Hivyo basi unatakiwa kufika hapa mahakamani kwa tarehe na saa ilyopangwa hapo juu bila kukosa wewe mwenyewe au wakili wako ukiwa na vielelezo vyote vya kesi hii.

Angalizo: Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itaweza kutoa uamuzi/hukumu kuwa wewe umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 26/8/2020.

RESIDENT MAGISTRATE
TEMEKE DISTRICT COURT

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE
DAR ES SALAAM.

215889802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matusi, kejeli kwenye kampeni havikubaliki

**NI** siku ya 14 tangu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ipulize kipenga kwa vyama 19 vyenye usajili wa kudumu kuanza kunadi sera zao kwa wananchi kwa ajili ya kuomba ridhaa ya kuchaguliwa katika ngazi ya udiwani, ubunge na urais, ifikapo Oktoba 28, mwaka huu.

Kiuhalisia tukifananisha kampeni na mtu aliyeshika kisu au panga ni kwamba wananchi wameshika kwenye mpini na wagombea kwenye makali, kwamba wananchi wakiamua kuvuta basi aliyeshika makali atakatikwa vidole.

Tayari Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha ACT-Wazalendo, Chama cha NCCR- Mageuzi vimeweka hadharani ilani zao, huku Chama cha Wananchi (CUF) kikizindua kampeni zake jana jioni na Chama cha CHAUMMA kilizindua Septemba 5, mwaka huu.

Ilani za vyama hivyo ziko kwenye tovuti, mitandao ya kijamii na kuna nakala zilizosambazwa, lengo ni kuwaonyesha wananchi kile watakachokisimamia kwa kipindi chote cha kampeni.

Baadhi ya wagombea wanaposimama kwenye majukwaa wanapanadi sera zao kushawishi wananchi, anasoma vipengele vilivyopo kwenye ilani zao na wanawaelewesha wananchi namna atakavyotekeleza.

Baadhi yao wanatumia majukwaa hayo vibaya kwa kudhalilisha wagombea anaoshindana nao kutoka vyama vingine, kiasi cha kutumia lugha za matusi ambayo hayastahili kutamkwa hadharani.

Sheria na kanuni za uchaguzi zipo wazi na zilisainiwa na vyama vyote kuwa vitahakikisha vinazisimamia, lakini baadhi wameanza kwenda nje ya mstari.

Kwa sasa dunia ni kama kijiji kwa kuwa mabadiliko makubwa katika upashanaji wa habari yamekaribisha uwapo wa uandishi wa habari wa kijamii (Citizen Journalism); kwamba mtu na simu yake na bando anarekodi kitu chochote na kurusha mtandaoni.

Kauli za kashfa na matusi zimekuwa zikirekodiwa na wananchi wenye simu zao na kusambaza, ikiwa na maana kuwa ndiyo ujumbe wagombea wameamua kuwafikishia wananchi wanaowaomba ridhaa ya kuongoza kwa miaka mingine mitano.

Baadhi ya wagombea wameacha kutumia nyenzo muhimu (Ilani) na sasa wanachanja mbuga kwenye matumizi ya lugha za ovyo bila kujali hadhira (umma) anaozungumza nao una mchanganyiko wa watu.

Kero na matatizo ya wananchi ni mengi sana na wanapofika kwenye mikutano anataka kusikia ni kwa namna gani anayeomba ridhaa atatatua au atawajibika kushirikiana nao kuleta maendeleo.

Inapotokea mgombea anatumia dakika 10 au 20 kumsema mgombea mwenzake, maana yake amefilisika kisera na sasa anatafuta tawi la kushika, na maana yake adhabu ambayo wananchi watampa ni kutomchagua.

Ni muhimu sana wagombea wakatumia vyema ratiba ya uchaguzi iliyotolewa na NEC kwamba unaposema utaanza kikao saa tisa au 10 jioni hakikisha umenadi sera zako kikamilifu ukieleza kwa kina jinsi ambavyo ilani ya chama chako inagusa maisha ya wananchi wote bila kuwabagua kwa rangi, kabila au itikadi zao.


Pia katika kampeni hizo zimesikika lugha za kibaguzi na vitisho kwa wananchi, jambo ambalo halipaswi kuwapo, kinachotakiwa ni mgombea kunadi sera zake na kushawishi wananchi.

Waelimisheni wananchi kutambua kilichomo kwenye ilani zenu, waelewe lengo kuu la kutaka kuongoza miaka mitano, kisha waacheni wafanye maamuzi ndani ya sanduku la kura.

Haya yote yanatokea na tunaamini NEC inaona na itachukua hatua madhubuti kwa wagombea kurudi kwenye mstari, lakini hali ikiachwa hivyo, itafika wakati itakuwa na mvutano ambayo utaweza kuteteresha misingi ya amani iliyopo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kufaulu kunahitaji ratiba ya kujisomea nyumbani

Na Sabato Kasika

**KILA** mzazi au mlezi, anapenda mafanikio ya mtoto wake. Tena afanye vizuri katika masomo na afaulu. Pia, walimu nao kwa upande wao wanajisikia vizuri wanapoona wanafunzi wao wamefaulu kikamilifu.

Lakini, mwanafunzi kufanya vizuri katika masomo hutegemea mambo kadhaa ambayo anatakiwa kuyazingatia, ikiwamo kuwa na ratiba ya kujisomea akiwa nyumbani ama shuleni.

Hatua hiyo, inamsaidia kufaulu mtihani na kumsukuma kufikia malengo aliyojiwekea kwenye elimu, kwa kuwa anapofaulu, huwa na mtazamo wa kujipeleka juu kielimu.

Katika kusaka elimu, wakati mwingine inakuwa ni vigumu kwa baadhi ya wanafunzi kumudu masomo na mitihani yao, wengine wakishindwa mitihani.

Wapo ambao wanafeli kwa sababu ya kutokuwa na ratiba ya kujisomea, badala yake wanapoteza muda kwa kucheza ama kutizama vipindi vya televisheni.

Ninaamini kwamba, baadhi ya wanafunzi wanaona ugumu kwenye masomo na kushindwa mitihani si kwamba hawana uwezo kiakili bali ni kutotenga muda wa kujisomea.

Kwa wanafunzi wa 'kisasa' naamini hawatengi muda ama ratiba, kwa kutegemea zaidi 'twisheni' wakiamini kwamba inatosha wakati bado wana nafasi ya kujiwekea muda wa kupitia kile walichojifunza.

Ikumbukwe kuwa kujisomea ni njia mojawapo inayomsaidia mwanafunzi kujiongezea uelewa wa mambo mbalimbali katika masomo, hivyo hilo siyo la kubezwa.

Tatizo hili la wanafunzi kutojisomea hata wawapo nyumbani ni mazoea, ambayo yanaweza kusababisha maendeleo duni ya kitaaluma.

Kuamini kwamba, 'twisheni' inatosha na kuona kuwa hakuna sababu ya kujisomea tena nyumbani, ni mawazo yasiyomfaa mwanafunzi anayejielewa anayetamani kuendelea zaidi kielemu.

Mwanafunzi anapotoka shule au 'twisheni', bado anatakiwa kutenga muda wa kujisomea nyumbani, kwa ajili ya kujiongezea uelewa.

Kwa hali kama hii ni wazi kwamba, wanaacha njia sahihi ambayo inaweza kuwasaidia kujiongezea maarifa, hivyo kuna haja ya kubadilika ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kuliona hili kuwaisaidia watoto wao.

Pamoja na kwamba mwanafunzi asome 'twisheni', bado kuna juhudi binafsi katika masomo, ambazo anatakiwa kuonyesha, hasa kutenga muda wa kutosha kujisomea awapo nyumbani ama shuleni.

Yapo baadhi ya mambo yanayotajwa na wataalamu wa elimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuyazingata ili kufanikiwa kielimu, ikiwamo kuweka lengo maalum la kusoma kila siku na kulitimiza.

Wanasema, ni muhimu kuwa na ratiba ya kila somo na kuifuata, mwanafunzi awe na mahali maalumu pa kusomea, kuepuka kitu chochote kinachoweza kumfanya usisome vizuri na asifanye mambo mengi kwa wakati mmoja.

Aidha, mwanafunzi hapaswi kufanya mapenzi ama anasa za kimwili wakati akiwa shuleni kwa kuwa hivyo ni vikwazo katika masamo na havitakiwi kuwa na nafasi kwa maendeleo ya elimu.

Vilevile anatakiwa kutafuta mahali pasipo na kelele na vurugu ili kuepuka vishawishi vinavyoweza kumfanye aahirishe kujisomea na kwamba kabla hujaanza kujisomea, ahakikishe ana ana zote muhimu kwa kusomea. Kama vitabu, maswali ya mazoezi na hata mtandao kwa ajili ya kuchimba zaidi.

Mbali na hayo, anatakiwa kuhakikisha kuwa mahali pa kusomea pana mwanga wa kutosha na anapokuwa na matatizo kimasomo, amwone mwalimu, mzazi au mlezi na asipoteze muda kwa mambo yasiyo ya lazima

Hayo ndiyo ya msingi ambayo mwanafunzi anatakiwa kuyazingatia, ingawa yawezekana kuna changamoto nyingi katika elimu, lakini nyingine ziko ndani ya uwezo wa wanafunzi wenyewe na wazazi wao.

Miongoni mwa hizo ni kutofuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, hali ambayo inawafanya watumie muda mwingi kuangalia televisheni, hata bila kukatazwa na kudhani hilo ni jambo la kawaida kuliko kujisomea.

Mwanafunzi awe anasoma 'twisheni', bado kuna juhudi binafsi katika masomo, ambazo anatakiwa kuonyesha, hasa kutenga muda wa kutosha kujisomea awapo nyumbani ama shuleni.

# TRA yaonya w'biashara wasio waaminifu

**Na Frank Maxmilian,** TUDARCo

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewaonya na kuwataka wafanyabiashara nchini kutumia namba ya mlipakodi (TIN) zao za biashara kwa usahihi wanapoagiza bidhaa nje ya nchi, na wasipofanya hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwenye vyombo vya habari na Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhende, mfumo uunganishi wa uondoshaji mizigo ya Forodha (TANCIS) umeboreshwa na kuweza kutambua namna ya mlipakodi.

Alisema mfumo huo utatambua namba ambayo haijatumika (iTIN) au isiyo ya biashara (nTIN), na kwamba hivi karibuni walibaini uwepo wa namba hizo zilizotumika na baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kuagiza bidhaa nje ya nchi na kuziuza nchini kinyume na matakwa ya sheria.

"Uboreshaji wa TANCIS pamoja na mambo mengine una lengo la kuiwezesha TRA kupata taarifa sahihi za kikodi kwa wamiliki wa TIN, ili kuhakikisha uhiari katika ulipaji kodi unafikiwa kwa kiwango cha juu kama ilivyo matakwa ya kisheria," alisema.

Dk. Mhede alisema TRA ilibaini kuwa kumekuwa na tabia ya kulipa kodi isiyo halali kwa namna mbalimbali miongoni mwa wafanyabiashara na wawekezaji wanaoingiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

"Baadhi yao wameonekana kulipa kinyume pasipo kufuata sheria na wengine kutumia iTIN na nTIN jambo lisilo jema kisheria," alisema.

"TRA inamsihi mtu yeyote mwenye dhumuni la kufanya shughuli yoyote inayohusiana na ulipaji kodi wajisajili na kupata TIN mapema, ili kuepusha usumbufu utakaoweza kujitokeza," alisisitiza.

Aidha, alisema hatua hiyo italeta faida kubwa zinazotokana na mzunguko wote wa bidhaa kuonekana kwenye ritani za kodi ya mapato.

Kwa upande wa ambao hawatatimiza wajibu au kupinga ulipaji kodi ipasavyo, watatakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria na kwamba itasimama kutetea usawa katika kulipa kodi za bidhaa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya uuzaji hapa nchini.

"Ni wazi kuwa TIN zinatolewa kwa wafanyabiashara wote ili waweze kutekeleza suala la ulipaji kodi nchini. Hivyo basi ni wajibu wa kila mfanyabiashara kulipa kodi ipasavyo pasipo kuangalia ni iTIN au nTIN. Inawapasa wafanyabiashara wote kuwa makini katika suala hili ili iweze kusaidia mamlaka ya mapato kufanya kazi kwa urahisi," alisema.

# TBS yanasa vipodozi hatari kwa binadamu

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limevikamata na kuondoa sokoni bidhaa za vipodozi zenye viambata vya sumu huku likiwaonya wauzaji wa bidhaa kama hizo nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TBS, Rhoida Andusamile, akizungumza na Nipashe jana kuhusu mchakato wa kuondoa bidhaa hizo katika Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam, alisema bidhaa zilizokamatwa zina thamani ya Sh. milioni 7.

Rhoida alisema wauzaji hao wanatakiwa kusajili majengo na bidhaa zao na kwamba katika soko la Kariakoo wamekuta vipodozi venye viambata vya sumu ambavyo haviruhusiwi kuuzwa nchini.

"Tumekamata wanauza bidhaa zenye viambata vya sumu, tumefuatilia na kuzuia na kuviondoa sokoni, na tutaviharibu. Mchakato huu ni endelevu tulishatoa tangazo wanatakiwa kusajili kutouza bidhaa hizo," alisema Rhoida na kuongeza:

"Bado wauzaji hawajasajili, wengine wanauza hadi mkorogo, tutafanya ukaguzi nchi nzima wa kuondoa bidhaa kama hizi sokoni."

"Watu hawa wamekuwa wakikiuka taratibu, hatuwezi kukaa kimya ndio maana tumekuja hapa kuviondoa ili kuhakikisha soko la Tanzania linakuwa na bidhaa bora zenye usalama kwa mtumiaji," alisema Rhoida.

Naye Mtathmini na Msajili wa bidhaa za vipodozi kutoka TBS, Ambumi Mwapeta, alisema wauzaji wa vipodozi wafike TBS kwa ajili ya kuzisajili bidhaa zao na kupewa maelekezo mengine ya kitaalamu.



Katibu Tarafa ya Somangila, Agusta Safari (kushoto), akizindua mradi wa maji uliotolewa na Taasisi ya Kiislam ya Dhi Nurayn Islamic (DIF), katika Mtaa wa Bamba, wilayani Kigamboni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wauza mbolea waagizwa bei elekezi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKAGUZI wa mbolea wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Christian Mhando, amewataka wafanyabiashara wa mbolea kuhakikisha wanauza mbolea yote kwa bei elekezi.

Mhando alitoa agizo hilo wakati anakagua maghala ya kuhifadhia mbolea na mawakala wanaouza mbolea katika maduka mkoani Ruvuma.

"Wafanyabiashara wahakikishe wanatoa risiti za mashine za kielektroniki baada ya kuuza mbolea kwa wananchi, pia wauze mbolea ambayo imesajiliwa na TFRA na kuzingatia utunzaji bora wa mbolea kwa kuwauzia wakulima mbolea yenye ubora... yeyote atakayekwenda kinyume cha maelekezo hayo atachukuliwa hatua," alisisitiza Mhando.

Aliwatahadharisha wafanyabiashara kuacha tabia ya kuuza mifuko ya mbolea ambayo imefunguliwa na kwamba TFRA itachukua hatua kali ikiwamo kuwanyang'anya leseni, kufunga biashara na kupelekwa mahakamani.

Katika Mkoa wa Ruvuma kuna kampuni saba za kununua mbolea na mawakala wa mbolea zaidi ya 120. Ofisa huyo alisema imebainika baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wanakiuka bei elekezi ya mbolea kwa kuongeza bei na kwamba changamoto hiyo imekuwa inajitokeza zaidi kwa wafanyabiashara wadogo.

Amezipongeza kampuni za uuzaji wa mbolea kwa kuzingatia bei elekezi na kwamba baadhi ya kampuni zimekuwa zinauza chini ya bei elekezi, hivyo kuleta unafuu kwa wakulima.

Amesisitiza kuwa bei elekezi za mbolea za Tanzania zimekuwa rafiki kwa wakulima ukilinganisha na nchi nyingine hasa katika kipindi hiki cha janga la corona ambapo imebainika bei ya mbolea ya Tanzania ni ya chini zaidi, hivyo kuleta unafuu kwa wakulima.

"Ukiangalia katika Mkoa wa Ruvuma katika msimu huu, mbolea ya kupandia bei yake haitazidi shilingi 50,000 kwa mfuko na mbolea ya kukuzia itakuwa kati ya shilingi 46,000 hadi 47,000 kutegemea na mazingira ambayo mkulima yupo," alisema Mhando.

Ofisa Kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Onesmo Ngao, aliwataka wakulima kuhakikisha wananunua mbolea yenye ubora na hasa katika kipindi hiki ambacho serikali imetoa bei elekezi ya mbolea katika Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla.

Ngao ameyataja mahitaji ya mbolea katika Mkoa wa Ruvuma kwa msimu ujao wa 2020/2021 ni tani 50,000, na kwamba serikali inaendelea kuhimiza kampuni za mbolea kuingiza mbolea, ambapo hadi sasa mbolea ambayo imeingizwa katika Mkoa huo ni zaidi ya tani 3,500.

# Mradi wa umeme Julius Nyerere kuwa wa kimataifa

**Na Hafsa Omar,** MOROGORO

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), utakamilika kwa wakati na kwa kiwango cha kimataifa.

Aliyasema hayo juzi kwenye ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa mradi huo unaotekelezwa Mto Rufiji.

Alisema serikali imeshamlipa mkandarasi wa mradi huo zaidi ya Sh. trilioni 1.49, ambayo ni sawa na asilimia 100 ya malipo ambayo mkandarasi huyo alitakiwa kulipwa kwa sasa, ili kuhakikisha anafanya kazi kwa kasi na kwa kiwango cha kimataifa.

"Tunataka mradi ukamilike kwa wakati na kwa kiwango cha juu, sio mradi unakamilika baada ya miezi miwili unaanza kuhitaji tena ukarabati kwa gharama nyingine kwa hili hatutakubali kwahiyo nitoe wito kwa mkandarasi kufanya kazi kwa weledi na kiwango cha juu," alisema.

Alisema, serikali inafuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huo, ili kuhakikisha mradi huo unakamilika ndani ya muda uliopangwa na kumtaka mkandarasi kuongeza kasi ya ujenzi.

Dk. Kalemani alitoa maagizo kwa mkandarasi pamoja na msimamizi kuwataka wataalamu wote waliofanya kazi kwenye mradi huo kufanya kazi kwa bidii na kumaliza kazi zao kwa wakati.

Pia, amemtaka mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha kuwa ifikapo mwisho wa mwezi Septemba awe tayari amemaliza ujenzi wa handaki.

Vilevile, amemtaka mkandarasi huyo kuajiri wataalamu wote ambao wanahitajika katika ujenzi na ifikapo mwisho wa mwezi wawe tayari wamefika nchini kwa ajili ya ujenzi huo.

"Hatuna wasiwasi na ajira zinazotelewa hapa kwenye mradi hadi sasa umeajiri Watanzania zaidi ya 4,500 kati ya Watanzania 5,500 na kwa wale waliobaki waajiri ili kazi ziweze kwenda kwa haraka," alisema Dk. Kalemani.

Pia, ameagiza uharakishwaji wa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi ambazo bado haujakamilika na kumtaka mkandarasi huyo kuzikamilisha haraka, ili wafanyakazi wa mradi huo wahamie katika eneo hilo zitakazo saidia wafanyakazi kufanya kazi zao kwa muda mrefu na mradi kukamilika mapema.

Naibu Waziri wa Ujenzi wa Misri, Jenerali Mahmoud Nassar, amesema Rais wa nchi yao anafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huo na yupo tayari kuhakikisha kuwa unakamilika kwa wakati.

Alisema kuwa mradi huo utakamilika kwa mafanikio makubwa kwa sababu ya ushirikiano mkubwa wanaopata kutoka kwa Watanzania, na kueleza kuwa utakapokamilika utaleta maendeleo makubwa nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, alisema maendeleo ya mradi huo ni mazuri na changamoto zilizojitokeza zitafanyiwa kazi na kuwataka Watanzania kuendelea kuunga mkono mradi huo wenye faida nyingi katika taifa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladislaus Mwamanga, akizungumza wakati wa kikao kazi cha kuwajengea uwelewa waandishi wa habari kutoka mikoa ya Shinyanga, Singida, Iringa na Dodoma, kuhusu utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya mpango wa kunusuru kaya maskini, jijini Dodoma jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Kabudi amuaga Balozi wa Iran

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano ]wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amemuaga Balozi wa Iran nchini, Mousa Ahmed Farhang, ambaye amemaliza muda wake wa uwakilishi.

Akizungumza katika hafla ya kumuaga balozi huyo jana jijini Dar es Salaam, Prof. Kabudi alimpongeza Balozi Farhang kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kudumisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi yake na Tanzania.

Pamoja na mambo mengine, Prof. Kabudi amemwahidi Balozi Farhang kuwa Tanzania itaendelea kushirikiana na Iran katika sekta za elimu, afya na utalii kwa maslahi mapana ya nchi zote mbili.

"Kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, nakuahidi ushirikiano kutoka kwetu, nakutakia kila la kheri katika maisha yako nje ya Tanzania na ni imani yangu kuwa utakuwa balozi mzuri wa Tanzania duniani," alisema Prof. Kabudi

Kwa upande wake Balozi Farhang aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kumpa ushirikiano wa kutosha wakati wa kipindi chake cha uwakilishi hapa nchini.

Balozi Farhang ameelezea kufurahishwa na uhusiano mzuri uliopo kati ya Iran na Tanzania na kupongeza hatua mbalimbali ambazo Serikali ya Tanzania imeendelea kuzichukua katika kuimarisha diplomasia ya uchumi.

# Mwapachu Mwenyekiti wa Bodi Benki ya Exim

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imemteua Balozi Juma Mwapachu kuwa mwenyekiti wake mpya wa Bodi ya Wakurugenzi, akichukua nafasi ya Said Mwema.

Mwema amemaliza muda wake kwa mafanikio kulingana na sera ya uongozi wa benki hiyo.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari jana, Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo imemshukuru Balozi Mwapachu kwa uongozi wake wa mfano na mchango wake akiwa kama Mkurugenzi katika Bodi hiyo tangu 2011 ikibainisha kuwa akiwa Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Balozi Mwapachu alihakikisha kuwa benki hiyo inaendelea kusonga mbele kimkakati na kiutendaji.



"Uzoefu wake mwingi, maarifa na uongozi aliouthibitisha utazidi kuipatia benki kasi ya kuendelea na ubunifu, kutafuta ukuaji wa baadaye, na kuimarisha zaidi msimamo wetu tukiwa miongoni mwa taasisi kubwa za kifedha nchini," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Jaffari Matundu, wakati akitoa maoni yake kuhusiana na uteuzi huo.

Balozi Mwapachu (pichani) ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi, Bodi ya Wakurugenzi, kampuni ya Heritage Insurance Tanzania Limited tangu 1998, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Alliance Life Assurance Tanzania Limited tangu 2014, ana uzoefu mkubwa akiwa amewahi kushika nyadhifa mbalimbali serikalini, katika mashirika ya umma, sekta binafsi na kwenye asasi za kiraia nchini Tanzania, kikanda na kimataifa.

Ana Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki (1969), Stashahada ya Juu katika Sheria za Kimataifa kutoka Chuo cha Indian Academy cha Sheria ya Kimataifa (1978), Udaktari wa Fasihi (Honoris Causa-2005) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Udaktari wa Sayansi ya Siasa (honors Causa 2012) kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Rwanda.

Balozi Mwapachu amewahi kuwa Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa (2002-Aprili 2006), Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Aprili 2006 - Aprili 2011) na Mwenyekiti wa Kamati ya Watendaji Wakuu katika Utatu wa COMESA-EAC-SADC (2008-2011). Pia Balozi Mwapachu amewahi kuwa Rais wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (SID) kutoka 2012-2016.

Kwa miongo kadhaa ya utumishi wake, ameongoza uanzishwaji wa taasisi mbalimbali ikiwamo Chemba ya Biashara Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki.

Wakati huo huo, Bodi ya Benki hiyo pia ilitangaza kumteua Irene Madeje-Mlola kama mjumbe mpya wa bodi.

HABARI KITAIFA

# RC awafunda walimu nidhamu ya mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, amewataka walimu kuwa na nidhamu ya fedha na uwekezaji.

Byakanwa alisema kwa kufanya hivyo itaepusha ukopaji usio na malengo kwa ustawi wa maisha yao na familia zao.

Aliyasema hayo katika kongamano la Siku ya Walimu 'NMB Teacher's Day 2020,' Kanda ya Kusini, mwishoni mwa wiki mjini Mtwara na kuwakutanisha NMB na walimu, lengo likiwa kusikiliza na kutatua changamoto zao, kupokea maoni yao na kuyafanyia kazi, pamoja na kuimarisha mahusiano baina ya benki hiyo na walimu.

Byakanwa alibainisha kuwa utafiti unaonyesha kwamba kumekuwa na utitiri wa mikopo isiyo na malengo miongoni mwa walimu na kwamba uwapo wa makongamano kama hayo, utamaliza changamoto hiyo.

Aliwataka washiriki kutumia vema elimu watakayoipata katika kongamano hilo kwa kujielimisha, lakini kushauri mambo yanayoweza kufanywa na benki hiyo, ili kuharakisha maendeleo yao, huku akiitaka NMB kuyasoma mazingira wanaoishi na kufanyia kazi walimu, ili kubuni huduma rafiki kwa maendeleo yao.

**Nyinyi ni kati ya watu mnaoongoza kwa mikopo isiyo na tija kwenu, hili ni jukwaa linaloenda kuwabadili iwapo mtatumia vema elimu hii.**

"Kumbukeni kuwa haya yanayofanywa na NMB yanaunga mkono juhudi za Serikali ya Rais John Magufuli, za kuwaunganisha Watanzania katika mifumo ya rasmi ya huduma za kibenki. Nyinyi ni kati ya watu mnaoongoza kwa mikopo isiyo na tija kwenu, hili ni jukwaa linaloenda kuwabadili iwapo mtatumia vema elimu hii," alisisitiza.

Aliongeza kuwa walimu ni kati ya makundi yanayoogopa sana suala la uanzishaji wa miradi ya maendeleo na uwekezaji mdogo, hivyo kuishia kutegemea mishahara yao, huku akiwaonya kutoshindana kukopa bila malengo, badala yake wajifunze uwekezaji katika sekta zinazowazunguka zikiwamo ufugaji, uvuvi, kilimo.

Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi na Kati wa NMB, Ally Ngingite, alimwahidi Byakanwa kuwa benki yake iko imara katika kusambaza elimu ya nidhamu ya fedha na kuwaepusha wateja wao na ukopaji hasi na kwamba fahari ya NMB ni kukopesha watu walioelimika kuhusu mikopo wanayohitaji.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, aliwapongeza walimu wanaofundisha mkoani Mtwara kwa kuuwezesha mkoa huo kushika nafasi ya pili kitaifa katika matokeo ya ufaulu wa kidato cha sita na kwamba kufanya kwao vema madarasani kunatokana na utulivu wanaopata kupitia elimu na mafunzo wanayopatiwa na NMB.

Aliunga mkono kauli ya Byakanwa kuwa kuna ukopaji usio na malengo kwa walimu na makundi mengine, lakini akaahidi kuendeleza kasi waliyonayo katika kuyapa elimu makundi yote kwenye jamii.

Sophia Luani, mwalimu kutoka Shule ya Msingi Tandika iliyopo Manispaa ya Mtwara, alibainisha kuwa walimu ni kati ya vinara wa ukopaji usio na tija kama ilivyofichuliwa na Byakanwa, lakini anaamini elimu waliyopewa inaenda kuwajengea fikra mpya katika kila mradi, biashara ama ujasiriamali watakaoanzisha.

Kwa upande wake, Ofisa kutoka Ofisi ya Elimu Halmashauri ya Tandahimba, Mukhaji Namangaya, aliishukuru na kuipongeza NMB kwa kongamano hilo, huku akisema nyakati za walimu kukopa wakiwa hawana elimu ya fedha na nidhamu ya fedha zimepita.

## THTU yaomba maboresho ya sheria

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), kimeiomba Ofisi ya Waziri Mkuu (Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) iendelee kuboresha changamoto za kisheria, kisera zinazopelekea mazingira magumu na kuongeza mzigo kwa wafanyakazi wa THTU.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Katibu Mkuu wa THTU, Elia Kasalile, kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa sita wa chama hicho uliofanyika mkoani Mwanza, ambapo wanachama takribani 120 wa chama hicho walishiriki, huku kauli mbiu ya chama hicho ikiwa 'Nia na mwelekeo wetu daima ni kujenga taifa kwanza'.

"Chama kinaendelea kutoa rai kwa serikali pamoja na mamlaka zake kwa ujumla kuendelea kuboresha sheria, sera na taratibu mbalimbali ili kupunguza changamoto zinazowakabili watumishi katika maeneo yao ya kazi kwani uwapo wa sera na sheria zinazohamasisha mazingira mazuri ya kazi zitapunguza mzigo mkubwa kwa watumishi," alisema Kasalile.

Mwenyekiti Taifa wa THTU, Dk. Paul Loisulie, alimwomba Mkuu wa Mkoa wa Mwanza awafikishie ujumbe kwa Rais John Magufuli kuwa menejimenti ya taasisi iache kuingilia majukumu ya vyama vya wafanyakazi kwani kutokana na menejimenti hizo kutana ziwekee mwakilishi kwenye vyombo hivyo.

Loisulie alisema taasisi za serikali zitoe ushirikiano wa ziada pale vyama vya wafanyakazi vinapokwenda kuzungumza nao na kujadiliana masuala yanayohusu maslahi ya wafanyakazi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ambaye alikua mgeni rasmi katika mkutano huo, alisema sekta hiyo ni nyeti, hivyo katiba yao inatakiwa ikifanye kuwa imara zaidi na kutoa mchango mkubwa kwa taasisi wanazotokana na taifa kwa ujumla.

Mongella amesema, taasisi za elimu ya juu bado zimejitenga na jamii, hivyo vyuo vinapaswa kushuka hadi chini kwa jamii ili kuipatia mawazo mapya ya kimaendeleo.

**Taasisi za serikali zitoe ushirikiano wa ziada pale vyama vya wafanyakazi vinapokwenda kuzungumza nao na kujadiliana masuala yanayohusu maslahi ya wafanyakazi.**



Mafundi wakikarabati taa za barabarani katika eneo la daraja la Selander, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Viongozi wa chuo watakiwa kulinda ubunifu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, amewataka viongozi wahakikishe wanafuatilia utaratibu wa kulinda ubunifu unaoibuliwa na wanafunzi chuoni hapo, ili ziwasaidie pindi wamalizapo chuo.

Prof. Mwakalila aliyasema hayo katika mahojiano maalum ya namna vyuo vinavyolinda ubunifu unaoibuliwa na wanafunzi vyuoni.

Alisema pamoja na utoaji wa elimu unaoendelea chuoni hapo kuanzia ngazi ya cheti hadi Shahada ya Uzamili, wamekuwa wakiwajengea uwezo na maarifa wanafunzi ili yawasaidie kuhimili ushindani wa soko la ajira mtaani.

Prof. Mwakalila alisema ni lazima vijana wajengewe uwezo tangu wadogo badala ya kutoka chuoni bila ya kuwa na ubunifu wowote.

Prof. Mwakalila alisema wameweza kupata vijana ambao wamebuni mifumo mbalimbali ambayo inahitajika kwenye jamii.

"Kuna kijana ametengeneza kifaa ambacho kinamwezesha mtumiaji wa jiko la gesi kujua kiwango cha ujazo uliopo na ikikaribia kuisha mfumo utampigia simu kumjulisha kiasi kilichobaki," alisema.

# Mil. 410/- kukarabati skimu umwagiliaji

**Na Renatha Msungu,** IRINGA

SERIKALI imesema itatoa shilingi milioni 410 kwa ajili ya kukarabati skimu za umwagiliaji mashamba yaliyoharibiwa na mafuriko mwanzoni mwa mwaka huu, kutokana na Mto Ruaha kuacha njia yake ya asili.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, wakati wa ziara ya kukagua uharibifu wa skimu za umwagiliaji za Pawaga na Ruaha Mbuyuni mkoani Iringa.

Kusaya alizitaja skimu ambazo zitanufaika na fedha hizo ni Mkombozi, Mlenge, Luganga na Magozi Wilaya ya Iringa zitakazopewa shilingi milioni 350 na skimu ya umwagiliaji Ruaha Mbuyuni itapewa shilingi milioni 60.

"Imenisukuma kuja hapa Pawaga kuona hali halisi ya uharibifu wa skimu zetu 4 za umwagiliaji zilizoharibiwa na mafuriko na kuwa Wizara ya Kilimo italeta shilingi milioni 350 mapema wiki ijayo ili kukarabati miundombinu," alisema Kusaya.

Akiwa katika skimu za Mkombozi, Mlenge, Magozi na Luganga Wilaya ya Iringa Katibu Mkuu huyo alisema atatuma wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na mitambo (greda) kurekebisha miundombinu hiyo iliyoharibiwa kufuatia Mto Ruaha mdogo kuacha njia yake ya asili.

**Imenisukuma kuja hapa Pawaga kuona hali halisi ya uharibifu wa skimu zetu 4 za umwagiliaji zilizoharibiwa na mafuriko na kuwa Wizara ya Kilimo italeta shilingi milioni 350 mapema wiki ijayo ili kukarabati miundombinu.**

"Nahitaji leo mitambo iwepo hapa Pawaga na wataalamu ili kazi ya kurejesha mto ianze na wakulima wapate maji kwenye mashamba yao," alisema Kusaya.

Kusaya aliwaambia wakulima wa mpunga kwenye skimu hizo kuwa serikali ya awamu ya tano ipo bega kwa bega kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinakuwa bora na kufanya kazi mwaka mzima, hivyo wakulima watoe ushirikiano kwa Tume kufanikisha ukarabati wa skimu.

Aliwahakikishia wakulima wa mpunga kwenye skimu hizo kuwa hakuna atakayechangishwa fedha bali serikali ndio itatoa fedha hizo kukarabati miundombinu ya umwagiliaji iliyoharibika na kuwa jukumu la wananchi ni kushirikiana na wataalamu kwa kazi ndogo ndogo kama kubeba mawe na mchanga kwenye maeneo ya kazi.

"Nataka ndani ya wiki moja kuanzia sasa wataalamu wa Tume ya Umwagiliaji mfanye kazi ya kuurejesha Mto Ruaha mdogo kwenye njia yake, vifaa na mitambo ipo. Wakulima wanachohitaji ni maji yafike kwenye mashamba yao haraka," aliagiza Kusaya.

Akiwa katika skimu ya umwagiliaji Ruaha Mbuyuni Katibu Mkuu Kusaya alijionea jinsi Mto Ruaha ulivyoacha njia zaidi ya mita 100 na kufanya banio kutokupitisha maji na wakulima kushindwa kulima zaidi ya hekta 450 msimu huu.

Aliwahakikishia wakulima hao kuwa Wizara ya Kilimo itafanya kazi ya kurejesha mto kwenye njia yake ya asili ili maji yafike kwenye mashamba ya wakulima kwa kuwa mto huo ndio tegemeo la wakulima kuzalisha mazao ya chakula yakiwemo mpunga, mahindi na mazao ya mboga (horticulture).

Akizungumza kwenye ziara hiyo mkulima Fundi Mihayo wa kijiji cha Luganga Wilaya ya Iringa, aliishukuru serikali kwa kuguswa na matatizo ya wakulima na kuchukua hatua.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Bashiri Mhoja, alisema mwaka huu wakulima walipata hasara kwa kuzalisha asilimia 2 tu ya zao la mpunga kutokana na miundombinu ya skimu za umwagiliaji kuharibiwa na mafuriko hivyo ameishukuru Wizara ya Kilimo kwa hatua ya kutoa fedha na wataalam kukarabati.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ruaha Mbuyuni Wilaya ya Kilolo, Hamis Matabazi, alisema wanakijiji wapo tayari kutoa ushirikiano kwa serikali kufanikisha urejeshaji wa Mto Ruaha mdogo kwenye njia yake kwani wana uhitaji mkubwa wa kuendelea na kazi ya uzalishaji mazao.




Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria (OUT), Felix Lugeiyamu (katikati) akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salam mwishoni mwa wiki, kuhusu uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu na kuwataka wananchi kuchagua viongozi bora, ili kuiletea nchi maendeleo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Wanafunzi wa chuo hicho, Edius Marcel na Ofisa Habari wa chuo hicho, Ruth Kyelula. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakulima Rukwa waahidiwa zana bora

**Na Mwandishi Wetu,** SUMBAWANGA

WAKULIMA mkoani Rukwa wameahidiwa zana bora za kisasa kupitia vyama vya ushirika.

Wamepewa ahadi hiyo na Kampuni ya AGRICOM Africa inayojihusisha na uuzaji na usambazaji wa zana za kilimo nchini.

Kampuni hiyo imewaeleza kuwa itawapa zana hizo kwa mkopo kabla ya msimu wa kilimo kuanza, ili waweze kufanya kilimo cha kisasa.

Akizungumza katika mafunzo ya matumizi bora ya zana za kilimo yanayoendelea katika wilaya za mkoa huo, Mkuu wa Ufundi wa Kampuni hiyo, Philipo William, alisema kampuni imeanzisha programu ya mafunzo ya matumizi ya zana ili kuwajengea uelewa wakulima juu ya umuhimu wa kutumia zana za kisasa katika uzalishaji.

"Lengo la kampuni sambamba na lile la serikali ni kuwatoa wakulima katika kilimo cha jembe la mkono na kufanya kilimo cha kisasa kwa kutumia zana bora ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao nchini jambo litakalosaidia kukuza uchumi," alisema William.

Alisema AGRICOM imejitosheleza kwa kuwa na zana zote za kilimo kuanzisha uaandaaji wa shamba, upandaji wa shamba, uvunaji na usafirishaji wa mazao hivyo kupitia vyama vya ushirika wakulima wanaweza kupatiwa zana hizo kwa mkopo kulingana na vigezo mbalimbali.

"Kwa kuchangishana nusu ya gharama ndani ya chama kampuni itawapatia zana hizo ikiwa ni matrekta ili waanze kutumia kwa kuandaa mashamba yao na pia kulitumia kwa kulimia mashamba ya wakulima wengine na kuwaingizia kipato ndani ya chama," alisema William.

Alielezea kuwa kuendelea kulitumia wataingiza kipato kitakachowezesha kumalizia deni na kufanya chama kipige hatua kiuchumi kwa kulitumia trekta hilo kwa shughuli mbalimbali na kuwaingizia kipato.

# Tathmini FCS yaridhishwa na taasisi Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

TAASISI inayotoa ufadhili kwa Jumuiya za kiraia Tanzania, The Foundation for Civil Society', imesema Jumuiya ya Tumaini Jipya Pemba 'TUJIPE' inaweza kuwa bora hapo baadaye kama changamoto ilizogundua wakati wa kijifanyia tathmini itazifanyia kazi haraka.

Hayo yalielezwa na meneja wa kuzijengea uwezo asasi hizo kutoka taasisi hiyo, Edna Chilimo, alipokuwa akizungumza na uongozi na wanachama wa Tumaini Jipya ofisini kwao Miembeni Chakechake, baada ya kumaliza kujaza dodoso la kujitathmini jumuiya hiyo.

Alisema changamoto ambazo waliziibua wenyewe wakati wa ujazaji wa dodoso, na kama wakizifanyia kazi, Tumaini Jipya inaweza kuwa jumuiya ya mfano hapo baadaye.

Alisema maeneo mengi jumuiya hiyo iko vizuri, ukiwamo uongozi na ufuatiliaji na changamoto kama za ukosefu wa usafiri, majengo ya kudumu, kutokuwa na tovuti na utaalamu mdogo wa uandishi wa miradi, ni mambo yanayoweza kufanyika.

Alieleza kuwa, zipo asasi za kiraia hazijafikia mafanikio kama yaliofikiwa na Tumaini Jipya, sasa ni wajibu wa viongozi na wanachama wao kubuni njia za kujiingizia kipato ili wapunguze changamoto.

"Mimi nimeona baada ya kumaliza zoezi la ujazaji wa dodoso la kujitathmini wenyewe, mnaweza kuwa na asasi kubwa ya mfani huko mbele, ila changamoto na kasoro mlizoziibua, ziondoweni,' 'alishauri.

Mwezeshaji binfasi kutoka Tanzania bara, Djaxb Iria, alisema njia ya kujitathmini kwa asasi yenyewe, huwapa ari na nguvu ya kuiendeleza upya.

"Njia hii ndio inayowezesha kampuni au asasi kujijua wako wapi katika kufikia malengo yao, hivyo na nyinyi Tujipe, sasa baada ya zoezi hili, mmeshaijua nafasi yenu," alieleza.

Akizungumza baada ya zoezi hilo, Mratibu wa TUJIPE Pemba, Tatu Abdalla Msellem, alisema wamefarajika kupata dodoso hilo, ambalo linawaonyesha wapi walipo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 8, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Ukurasa 13

**Beking poda ilivyo na mengi**



Ukurasa 14

Miaka mitano ilivyobadili sura ya taaluma kimkoa



Ukurasa 12

**Siku waziri alipowaonyesha ajira ya kilimo wahitimu vyuo**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Elimu yasikika ‘kampenini’ japo inazongwa na mengine



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakijisomea kwenye vimbweta au viti vya zege.
**PICHA: MTANDAO**

KIPAUMBELE cha elimu kimejitokeza kwa nguvu ya hoja kwenye kampeni za kuwania urais uchaguzi mkuu wa mwaka huu. Hata hivyo, siyo rahisi agenda hiyo kutawala majukwaa kwa muda mrefu.

Kwa upande fulani ni upinzani ambao umeangalia kwa karibu zaidi suala la elimu, wakigusa maeneo kadhaa ambayo yanaweza kuinua hisia za kutaka mabadiliko miongoni mwa wapigakura na siyo ajabu ajenda hiyo ikasikika zaidi siku zijazo.

Ni eneo ambalo limewahi kuleta mijadala mikali bungeni na kuundwa tume au kamati, serikalini kubadilisha mambo na mfumo mpya kutangazwa 2015.

Mijadala ya elimu ina tatizo la nini hasa kipaumbele katika sekta hiyo kwani elimu ni ngazi au daraja la kutoka tabaka moja kwenda jingine kwa jadi, ila kibano cha kupatikana ajira tangu mwanzo wa karne mpya kumeifanya kupoteza ubora huku uwezeshaji kiuchumi ukichukua kipaumbele.

Elimu ndiyo msingi wa kila kitu kwani bila elimu bora watu hawawezi kuwezeshwa endapo hawataweza kujifunza kinachohitajiwa na kwa maana hiyo elimu ya msingi hadi sekondari imekuwa kipaumbele muhimu nyakati za uchaguzi.

Ni muhimu kuwa elimu kwenye kampeni kwani ni eneo ambalo lilivutia wapiga kura mwaka 2015 na kufanyiwa kazi. Licha ya kuwa na umuhimu zaidi mfumo wa elimu ni ngazi ya elimu ya msingi, inaelekea kuwa kuanzia sekondari hadi vyuoni ndiyo sehemu inayoleta hamasa katika majadiliano, na ndiyo ilivyo katika hatua za awali za mijadala ya sera.

Hakuna malengo mapya yaliyosikika kuhusu elimu ya msingi kwani mpango wa elimu bure tayari upo na unetekelezwa kutoka msingi hadi sekondari ila kuna wagombea wameanza kutaja umuhimu wa elimu bure hadi vyuo vikuu.

Kuna wakati ACT-Wazalendo ilieleza ulazima wa kufuta na kusamehe mikopo elimu ya juu.

Eneo jingine ambalo limeguswa katika mapendekezo ya sera ni kupanua ajira katika elimu, kama sehemu ya kuongeza kazi za wataalamu kwa jumla, elimu ikiwekewa mkazo maalum.

Ni mwelekeo wenye kusisitiza katika ajira za walimu kuongeza ufanisi kwenye kufundisha na mitaala iboreshwe kwa jumla, licha ya kuwa mkazo unatakiwa ngazi ya sekondari kwani wahitimu wake kama walivyo wa vyuo vikuu wanaokosa ajira.

Suala la ubora wa elimu halijasikika sana katika majukwaa kwani limekaa kitaalamu zaidi; linajadiliwa bungeni kila wakati.

Wanaharakati wa kijinsia wanaweza wakahisi kuwa wagombea urais wamekwepa kuzua zogo kuhusu sera ya kutorudi shuleni kwa wasichana wanaopata mimba wakiwa kwenye ngazi ya msingi na hasa sekondari.

Jambo hilo lilileta mjadala mkali miaka takriban mitatu iliyopita na kutafutiwa majawabu kwa kina, hasa kupatikana kwa njia mbadala za kukamilisha ngazi ya elimu.

Hivi sasa halipo mezani katika mijadala kati ya serikali na mashirika ya kimataifa na hasa kwa upande huo Benki ya Dunia.

Kuna wakati Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliizua mjadala alipounga mkono na kupeleka barua makao makuu ya WB Washington, kutaka serikali isipewe fedha kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu kutokana na kubaguliwa wasichana wanaopata mimba. Baadaye zogo hilo lilimalizika na kwa hali yoyote ile liligusa zaidi hisia za wanaharakati halikuwasha moto bungeni, kwani kimsingi linaendelea kuwagusa wengi.

Licha ya kwamba wagombea urais upinzani pia ni wanaharakati wa masuala ya jinsia na elimu kwa wasichana, ilibidi wasiyatangulize.

Kimsingi suala la elimu limekuwapo katika hisia za wagombea urais wa vyama vikubwa na hasa vya upinzani, ikikumbushia jinsi jambo hilo lilivyoibuka mwaka 2015,mgombea wa CHADEMA akisema ‘kipaumbele cha kwanza ni elimu, cha pili ni elimu na cha tatu ni elimu.’ Haitazamiwi tangazo kama hilo kutolewa uchaguzi mkuu wa sasa kutokana na mabadiliko mengi ambayo yametokea miaka mitano iliyopita.

Maeneo ambayo hayajafanyiwa kazi siyo rahisi kuyajadili katika kadamnasi kwani yana unyeti wa kitaaluma, hayagusi watu wengi na pia hayana majawabu rahisi kama inavyotakiwa katika kutoa sera za chama fulani.

Ni mapendekezo kadhaa tu ambayo yamefikishwa kwa wapigakura kutafakari, hasa kupeleka elimu bure hadi kufuta mikopo ya elimu ya juu.

Inawezekana baada ya kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaendelea sasa serikali inaweza kuanza kuangalia eneo hilo, hasa kwa kulinganisha gharama za utoaji na urejeshaji wa mikopo au uendeshaji wa bodi inayohusika na urejeshaji halisi.

Bado hakuna utafiti wa kina nini hasa mwelekeo wa kurudisha fedha, lakini mazingira ya kukosa kazi kwa miaka kadhaa baada ya kuhitimu, kutokuwapo na ajira halisi zinazofahamika serikalini kijana akishahitimu na mishahara midogo wanayopata wahitimu inagusa uwezo wa kurejesha mikopo kwa ufanisi.

Endapo itadhihirika kuwa usimamizi wa kutolewa na kurudisha mikopo ni gharama kubwa zaidi ya hayo mapato yaliyopatikana, huenda sera hiyo ikarasimishwa, wataalamu wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu wakatazama namna bora ya kufanya kazi hiyo.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Siku waziri alipowaonyesha ajira ya kilimo wahitimu vyuo



Wahitimu wa vyuo vya kilimo wanaweza kunufaika wakijikita vijijini na kujishughulisha na kilimo kama hiki. **PICHA: MTANDAO**

KILIMO kinatajwa kuwa ndiyo sekta pekee nchini pengine na duniani ambayo haibagui mtu. Haijali kama mkulima amesoma au ni mbumbumbu, kwa hiyo ndilo kimbilio la kila anayetaka kujiajiri na kutajirika.

Kinasifiwa kuwa ni kazi iliyotukuka. Ndiyo mwanzo wa afya kwa kuwa kila kinacholetwa mezani au dawa za kutibu maradhi chanzo chake ni shamba.

Bidhaa nyingi za viwandani malighafi zake ni shambani ziwe nguo ni kazi ya pamba, viatu ni zao la ngozi na mifugo, mapambo yakiwamo mazulia ni lazima mkonge utahusika, wakati mafuta na vilainishi vya mitambo kilimo kinavizalisha vikitokana na mnyonyo.

Sekta ya kilimo inaweza kufananishwa mhimili wa uchumi duniani, kutokana na fursa zilizopo, Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, anawataka wahitimu wa vyuo vya kilimo nchini, kuchangamkia fursa zilizopo kuendeleza kilimo vijijini ili walete maendeleo yao na ya jamii.

Anatoa ushauri huo wakati akifungua kongamano la vijana wakulima mkoani Arusha na kuwahamasisha kufanya mabadiliko kwa kuwa Tanzania ina takribani vijana milioni 16.1 sawa na asilimia 35 ya idadi ya wananchi wote, hivyo wakifanya jambo lazima litakuwa na matokeo makubwa.

Anasema hana nia ya kuwazuia kusaka ajira rasmi bali anataka kuwaonyesha ni namna gani wanavyoweza kutumia utaalamu walionao kwa ajili ya kuchangamkia fursa zilizopo vijijini kuendesha maisha yao badala ya kukimbilia kuajiriwa muda wote.

Naibu Waziri anasema, kilimo ndiyo sekta pekee ambayo haibagui mtu aliyesoma na asiyesoma, kwa kuwa kinahitaji elimu kiasi na ni njia ya kupata utajiri hivyo wasomi nao waingie katika sekta hiyo na kujibidisha.

Anasema, wahitimu wa vyuo vya kilimo, wanaweza kunufaika iwapo watakwenda vijijini kuanzisha mashamba ya mfano na kutoa elimu kwa wakulima jinsi ambavyo wanaweza kulima kwa tija.

"Kwa sasa wapo baadhi ya wakulima vijijini, ambao wako tayari kulipia gharama za utaalamu wa kilimo, lakini maofisa ugani na wataalamu hawapatikani, kwa hivyo vijana wasomi changamkieni fursa hiyo," anawashauri Mgumba.

Mgumba anasema, hapa nchini kuna uhaba wa maofisa ugani, hivyo wasomi hao wanatakiwa kwenda vijijini kutoa elimu kwa wakulima na kujipatia fedha kuliko kuzunguka na vyeti kutafuta ajira wakati zimejaa vijijini.

Aidha, anasema, kuna mkakati wa taifa wa miaka mitano kwa vijana kushiriki katika sekta ya kilimo wa mwaka 2016/17 hadi 2020/21, ambao utekelezaji wake unahusu masuala ya ardhi ya kilimo.

"Mkakati huo pia unahusu kupata pesa kwa ajili ya kilimo, pembejeo na zana za kilimo, masoko ya mazao, kukabili mabadiliko ya tabianchi na ujasiliamali," anasema.

Anaeleza kuwa serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa vijana, na tayari inatekeleza mkakati wa kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa.

Anafafanua kuwa takwimu zinaonyesha upotevu wa mazao yasiyo ya nafaka ni asilimia kati ya 30 hadi 40 na hiyo ni hasara kwa mkulima.

**UHABA WA MAOFISA**

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Andrew Komba, akizungumza katika kongamano hilo anathibitisha kuwa kuna uhaba wa maofisa ugani.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa maofisa ugani kutoka mikoa mbalimbali uliohudhuriwa pia na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, anasema, Tanzania ina vijiji 12,400, na kuna idadi ndogo ya maofisa ugani.

**UHABA WA WAGANI**

Komba anaeleza kuwa idadi hiyo haitoshelezi mahitaji ya huduma za ugani kwa vijiji vyote, hivyo ipo haja ya kuhakikisha kila kila kijiji kinakuwa na wataalamu.

> "Kwa upande wa wataalamu wa mifugo na uvuvi, wapo 419, ambao kwa ujumla wao hawatoshelezi kwa idadi ya vijiji vilivyopo nchini, hivyo ni muhimu kila kijiji kuwa na mtaalamu," anashauri Komba.

Anasema kuna maofisa ugani 7,307 wanaotoa huduma za kilimo na mazao 3,795 pekee, idadi ambayo haitoshelezi mahitaji ya huduma za ugani kwa vijiji vyote, hivyo ipo haja ya kuhakikisha kila kila kijiji kinakuwa na mtaalam.

"Kwa upande wa wataalamu wa mifugo na uvuvi, wapo 419, ambao kwa ujumla wao hawatoshelezi kwa idadi ya vijiji vilivyopo nchini, hivyo ni muhimu kila kijiji kuwa na mtaalamu," anashauri Komba.

Katika hilo, anasema, wakulima wengi nchini wanalima kilimo cha hasara kisichozingatia matumizi sahihi ya ardhi na maji, hivyo kuna umuhimu wakulima wote kufikiwa na elimu.

Kwenye mkutano huo, inaelezwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga kwamba ni kutokana na asilimia 80 ya wakulima nchini kuwa kiwango chao cha juu ni darasa la saba.

"Kuna umuhimu kwa maofisa ugani kuhakikisha kuwa wakulima hao wanapatiwa mafunzo ya kilimo ili waweze kuondokana na kilimo cha hasara na kuzalisha kwa tija ili wanufaike," anasema Hasunga.

Baadhi ya vijana wanakiri kuwa uhaba wa ajira, ni moja ya changamoto inayowakabili wahitimu wa vyuo mbalimbali, hali ambayo inasababisha wazunguke katika ofisi za umma na binafsi kutafuta kazi.

Katika kongamano hilo wanasema kuwa imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi yao kutoka fani mbalimbali, kukaa kusubiri ajira badala ya kujiongeza kwa kutumia fursa zilizopo kwa kutumia elimu walionayo kujiajiri.

Wanasema kuna haja na kutambua kwamba, kuna suala la uhaba wa ajira nchini, ambalo kijana msomi hatakiwi kubweteka kwa kuendelea kuzungukia ofisi kusaka ajira.

Ndivyo vijana wasomi wanavyoshauriwa na viongozi wa serikali akiwamo Waziri Hasunga kwamba wakati huu wa sayansi na teknojia, lazima wabadilishe fikra za utamaduni wa kusubiri kuajiriwa na badala yake watafute maarifa ya kujiajiri.

Wanashauriwa kuwa wabunifu na kutumia usomi wao kutatua tatizo la ajira kwa kuacha kufikiria zaidi kuajiriwa na serikali au kampuni na viwanda kwani siyo rahisi wote wakaajiriwa kutokana na hali ya uchumi na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ambayo inasisitiza kutumia zaidi mashine badala ya mikono ya binadamu.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# ‘Beking poda ilivyo na mengi’

## ■Ni tiba meno, kiungulia, ngozi
## ■Humaliza viuatilifu kwenye mboga




NI maarufu kama ‘beking poda au soda’ ambayo wengi wanaopika vitafunwa kama maandazi, bajia, keki na mikate wanaifahamu. Pengine ni kiungo ambacho karibu kila nyumba hasa mijini inakitumia.

Beking poda inatajwa kuwa na manufaa mengi takribani 23 mbali na kutumiwa kuandaa vitafunwa ina matumizi mengine mengi kama kutibu magonjwa mbalimbali mathalani ...

**DAWA YA KIUNGULIA**

Kiungulia ni tatizo linaloitwa kitabibu ‘acid reflux. Baadhi ya sababu za kiungulia ni msongo wa mawazo, vyakula vyenye ukakasi kama ndimu, maziwa mtindi na chakula chenye viungo vingi. Aidha, ukiwa na vimelea kama ‘helicobacter’ navyo pia huongeza tindikali na kusababisha kiungulia.

Beking soda inapotumiwa kiasi cha kijiko cha chai kwenye glasi ya maji na kuchanganywa kikamilifu, mwenye kiungulia anapotumia taratibu anapona tatizo hilo endapo limetokana na chanzo ambacho si kuwa na vimelea tumboni. Hata hivyo, si dawa ya kunywa kila siku kwani inaweza kukuletea madhara ni vyema kuwasiliana na madaktari.

**HUSAFISHWA KINYWA**

Ukitumia kiungo hicho ni sawa na kusukutua ‘mouthwash’ dawa ya maji ambayo inapotumika hukamilisha kazi ya kuondoa harufu mbaya kinywani kwa vile inafika sehemu zote kuanzia meno, fizi, ulimi, kaa kaa la juu ya kinywa na kule ambako mswaki haupiti.

Wengi hutumia kiungo hicho kama mbadala wa dawa ya meno, baadhi ya watafiti wanasema inasafisha mdomo na kuleta harufu nzuri kinywani na pia ni tiba ya kuua vimelea vinavyojificha na kushambulia meno na fizi. Hata hivyo, haimaanishi kuwa watu wasipige mswaki na dawa ya meno.

Ni vyema kuswaki na dawa na kitaalamu unashauriwa kuweka dawa ya kutosha inayolingana na ukubwa wa brashi za mswaki na kusafisha kinywa angalau mara tatu kwa siku.

Iwapo utatumia tiba hii, kipimo kinachoshauriwa ni nusu kijiko cha beking poda kwenye nusu kikombe au glasi ya maji ya moto baada ya kuchanganya anza kusukutua kwa dakika kadhaa.

**KUTIBU VIDONDA**

Inatumiwa pia kutibu vidonda vidogo vinavyosumbua kinywa. Unaweza kutumia nusu kijiko cha chai kwenye nusu glasi ya maji ya uvuguvugu kila siku hadi vidonda vitakapotoweka.

Pamoja na kuponya vidonda hung’arisha meno na kuondoa utando wa njano au rangi ya kufubaa kwenye meno. Beking poda huyafanya meno kuwa meupe na yanayong’ara zaidi.

**KUTIBU VIUATILIFU**

Beking poda ikitumiwa husafisha na kuondoa sumu au mabaki ya viuatilifu kwenye matunda na mboga.

Ni muhimu kwani watu wengi wanahofu kula nyanya au zabibu zenye dawa. Lakini ni lazima wakulima kuweka dawa ili kuzuia wadudu waharibifu. Kwa upande wa matunda kumenya ni kuondoa dawa au sumu inayobakia kwenye ganda, lakini mboga hazimenywi.

Hata hivyo, ukimenya unaondoa viinilishe kama nyuzinyuzi (fibers), vitamini, madini na virutubisho vingi vinavyopatikana kwenye ganda. Kwa hiyo ili kumaliza mabaki ya sumu mlaji anashauriwa kuloweka matunda na mboga kwenye beking soda ili kuondoa masalia ya kemikali hizo.

Utafiti wa karibuni unaonyesha kuwa kuloweka epo au tufaa kwenye maji yenye beking soda kwa dakika takribani 15 huondoa sumu ya viutilifu kwenye maganda. Lakini njia hii haizimalizi sumu zilizomo ndani ya tunda bali ile iliyoko kwenye maganda. Kwa hiyo ni vyema kula matunda na mboga zenye viuatilifu asilia.

**DAWA YA MAGUGU**

Beking poda au soda inaweza kutumiwa kuua magugu au majani yanayootoa kwenye bustani na kusambaa kwa kasi huku ikiua mazao yanayopandwa.

Badala ya kutumia viua magugu (weed killers) tumia beking soda kama mbadala wa kemikali kwa kunyunyuzia magugu hayo. Lakini, ni vyema kuwa makini kwani inaweza kuua hata mimea kama maua na mboga iwapo itatumika kwa wingi na bila kukinga mimea unayoihitaji.

**‘NI DEDORANT’**

Watu hutumia manukato kama ‘pafium’ na ‘deodoranti’ kuondoa harufu mbaya ya jasho kwenye makwapa, lakini utafiti unaonyesha kwamba beking poda inaondoa harufu na huna haja ya kupaka deodoranti’ ambazo zina athari mwilini.

Kinachofanyika ni kama vile kutumia poda paka kiungo hicho na sugua makwapa kikamilifu kila wakati unapooga na utaona harufu ya jasho kali ya kwapa ikiondoka bila gharama kubwa.

**DAWA YA NGOZI**

Kuogea kiungo hiki kunasaidia kutibu ngozi inayowasha na hasa pale mtu anapoumwa na wadudu kama kunguni, chawa na manyigu au nyuki. Pia, ikichanganywa na dawa nyingine inasaidia kuondoa mabaka meusi na mekundu yanayosababishwa na kuungua jua.

> Ni vyema kuswaki na dawa na kitaalamu unashauriwa kuweka dawa ya kutosha inayolingana na ukubwa wa brashi za mswaki na kusafisha kinywa angalau mara tatu kwa siku.

Unaweza kujitibu sehemu zilizoumizwa kwa kuweka vijiko hadi viwili vikubwa vya beking poda kwenye maji ya uvuguvugu kiasi na kuiloweka sehemu iliyong’atwa au kuumwa na mdudu.

Lakini pia, unaweza kuiweka kwenye maji na kuitengeneza ‘tope’ ukiibandika sehemu iliyoumia.

**MARADHI YA FIGO**

Wagonjwa wa figo au chronic kidney disease (CKD), wanaweza kupata matatizo ya figo kushindwa kufanyakazi.

Figo ni muhimu kwani pamoja na kuchuja mwili na kuondoa maji ya ziada mwilini zinahusika na kuweka uwiano wa madini muhimu mwilini kama potasiam, sodiam na calcium (kalisi).

Utafiti uliofanywa kati ya watu wazima 134 wenye CKD ulibaini kuwa waliotumia beking soda asilimia 36 haikupata matatizo ya maumivu makali na ugonjwa ulipungua wakati wale ambao hawakuigusa walibanwa na ugonjwa zaidi.

Hata hivyo wagonjwa wa figo wanashauriwa kwenda hospitalini na kuwasiliana na wabobezi badala ya kukimbilia kunywa kiungo hicho cha kupikia mikate na vitafunwa.

**HUPUNGUZA SARATANI**

Kiungo hiki kikitumiwa na wagonjwa wa kansa ambayo inatajwa kuwa ni chanzo cha vifo vingi duniani, bila kujali ni wa kutoka nchi maskini au zenye uchumi mkubwa.

Saratani ambayo hutibiwa na ‘chemotherapy’ dawa zinazopunguza kasi ya ukuaji wa seli za kansa mwilini au hata kusimamia ukuaji wake, inaweza pia kupunguzwa makali kwa kutumia beking poda.

Kinachofanyika ni kusaidia kuweka uwiano wa juu wa nyongo kuliko tindikali (alkaline na acid). Beking inaongeza mazingra ya kuwa ya nyongo au alkaline zaidi na kuirahisishia tiba ya ‘chemotherapy’ kufanyika kwa ufanisi zaidi kwa vile mazingira ya tindikali ndiyo yanayosaidia kuimarisha seli za kansa.

Hata hivyo, utafiti unahitajika zaidi na kuwa na ushahidi wa kutosha hivyo, haina maana kuwa wagonjwa wakimbilie beking poda badala ya kwenda kwa wataalamu.

**DAWA YA MADOA**

Inapotumiwa kikamilifu huondoa madoa jikoni kwenye majiko ya gesi au ya umeme. Huondoa harufu kwenye friji. Ukitumia kwenye oven, vikombe vilivyochafuka kwa rangi ya kahawa, au chai ya majani mengi, marumaru zilizofubaa bafuni au popote, bila kusahau jiko la ‘microwaves’ ikitumiwa ipasavyo huondoa madoa na kurudisha mng’aro wa vifaa au sehemu hizo.

***MTANDAO HEALTHLINE***

ELIMU

**NA JOHN MAPEPELE, SINGIDA**

# Miaka mitano ilivyobadili sura ya taaluma kimkoa

"ELIMU ni silaha yenye nguvu kuliko zote unayoweza kutumia kubadilisha dunia" ni maneno aliyoyatoa aliyekuwa Rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, akisisitiza umuhimu wa elimu ili kuwa na taifa lenye maendeleo na mapinduzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Aidha, Mwalimu Julius Nyerere, baba wa taifa anaongeza kusema, "njia bora ya kuwapa pesa maskini ni kuwapa watoto wao elimu bora."

Kwa misingi hiyo awamu ya tano ya Rais John Magufuli, inahitimisha miaka mitano kufanya mapinduzi na mageuzi makubwa katika sekta ya elimu hali inayowafanya wananchi wengi wenye kipato kidogo kumudu kusomesha watoto wao.

Hali hiyo ni matokeo ya Sera ya Elimu Bure ambayo inasisitiza watoto wenye umri wa kuanzia miaka sita kuanza shule za msingi mara moja.

"Hii ndiyo imetuwezesha kuboresha huduma mbalimbali za jamii na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, ambapo kwa upande wa huduma za jamii tumepanua wigo na kuboresha upatikanaji wa huduma za elimu, afya pamoja na maji. Kwenye elimu kama unavyofahamu, tulianza kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari ambapo mpaka mwezi Februari 2020 tulikuwa tumetumia Sh. trilioni1.01 kuigharamia," anasema Rais Magufuli.



Mkuu wa Mkoa wa Singida (kulia), Dk. Rehema Nchimbi, akizungumzia mafanikio ya kielimu katika mkoa huo yaliyopatikana ndani ya miaka mitano. **PICHA: MTANDAO**

Ni katika hotuba yake ya kuliahirisha bunge Dodoma Juni 16, 2020, anapobainisha kuwa mbali na kugharamia elimu katika kipindi cha miaka mitano serikali imeongeza shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka huu na sekondari kutoka zimefikia 5,330 mwaka huu wakati zilikuwa 4,708 mwaka 2015.

Aidha, shule kongwe 73 zimekarabatiwa kati ya 89, yamejengwa mabweni 253 na vyumba vya maabara 227, serikali imepunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa madawati na kwa miaka mitano yameongezeka kutoka 3,024,311 mwaka 2015 hadi kufikia 8,095,207, Rais anawaeleza wabunge.

Kwa upande wa vyuo vya ualimu, serikali imevikarabati 18, imejenga upya vyuo viwili Muruntunguru na Kabanga na kupeleka kompyuta 1,550 kwenye vyuo vyote 35 vya ualimu kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Rais anasema Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi (VETA) vimeongozwa kutoka 672 mwaka 2015 hadi 712 mwaka 2020 na pia imekarabati na kuboresha vifaa na miundombinu ya kufundishia katika vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (FDC).

Kutokana na hatua hizo, uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza umeongezeka maradufu kutoka wastani wa watoto 1,000,000 mwaka 2015 hadi milioni1.6 hivi sasa.

Aidha, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi nne imeongezeka kutoka milioni 1.64 mwaka 2015 hadi milioni 2.18, huku wanaosoma ufundi VETA wakongezeka kutoka 117,067 mwaka 2015 hadi 226,767 mwaka 2020 na wa FDC sasa ni wanafunzi 9,736 mwaka 2018/19 kutoka 6,693 mwaka 2016/17.

Kwa upande wa vyuo vikuu wanaojiunga mwaka wa kwanza imeongezeka kutoka 65,064 mwaka 2015, hadi 87,813 mwaka 2020 na wanaopokea mikopo mwanzoni walikuwa 98,300 mwaka 2014/2015, lakini sasa ni 130,883 rekodi za mwaka 2019/2020, kwa mujibu wa Rais Magufuli.

> Ni katika hotuba yake ya kuliahirisha bunge Dodoma Juni 16, 2020, anapobainisha kuwa mbali na kugharamia elimu katika kipindi cha miaka mitano serikali imeongeza shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka huu na sekondari kutoka zimefikia 5,330 mwaka huu wakati zilikuwa 4,708 mwaka 2015.

**ELIMU SINGIDA**

Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Nelasi Mulungu, akizungumzia mafanikio ya elimu mkoani hapa anasema umetekeleza wa miradi ya maendeleo ya miundombinu ya elimu yenye thamani ya Shilingi bilioni 24.076 ikijumuisha ununuzi wa pikipiki za maofisa elimu kata zote.

Aidha, mkoa ulipokea Sh. bilioni 28.5 5 kutekeleza programu ya elimu bila malipo na kupata mafanikio ya elimu hususani kusajili wanafunzi wa madarasa ya awali na darasa la kwanza.

Halikadhalika shule za msingi na sekondari na miundombinu ya mawasiliano imeongezeka na kwamba ubora na upatikanaji wa elimu kuanzia ya awali hadi kidato cha sita umeimarika, anasema Mulungu.

Ofisa Elimu Mkoa anafafanua kuwa katika kipindi cha kuanzia 2016 idadi ya shule za msingi zimeongezeka kutoka 507 hadi 575 mwaka 2020, shule za sekondari zimeongezeka kutoka 159 mwaka 2016 kufikia 167mwaka 2020,vilevile serikali ilitoa vitabu kwa shule 993,200 za awali, msingi na sekondari.

Anasema Singida inaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kutoa elimu bora kwa wanafunzi wa msingi na sekondari na kipaumbele cha mkoa ni kuongeza ufaulu katika mitihani yote, kuboresha miundombinu, kupambana na utoro, kuongeza samani na kuimarisha ufundishaji katika mamlaka za serikali za mitaa. Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 1995 kila shule ya msingi ni lazima iwe na darasa la awali.

Anaongeza kuwa walimu na wadau wote wa elimu wanapaswa kushirikiana ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa kuwa serikali tayari imeshatekeleza wajibu wake wa kuwawezesha kwa kiasi kikubwa.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, anapongeza jitihada za Rais Magufuli za kuwezesha sekta mbalimbali akisema uwezeshaji umekuwa wa kiwango cha juu kinachotakiwa kufanyika kwa sasa ni watumishi wa serikali kuunga mkono juhudi hizi kwa vitendo.

Dk. Nchimbi anafafanua kwamba Mkoa wa Singida umejiwekea kauli mbiu ya mwaka huu isemayo "Timiza Wajibu Ongeza Ufaulu" anasema na kuwataka walimu kusimamia viapo vyao na kuongeza mafanikio katika taaluma.

Mwandishi wa Makala haya ni Ofisa Habari Mkuu wa Mkoa wa Singida

***Maoni jmapepele1@gmail.com, 0784 44 11 80***



# Wahandisi chipukizi wapigiwa chapuo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, ameziteka wizara na taasisi za serikali kuwatumia wahandisi wanaohitimu kwenye vyuo mbalimbali nchini ili kuchangia maendeleo ya Taifa.

Mhandisi Sanga, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati akifunga Mkutano wa 17 wa Maadhimisho Siku ya Wahandisi.

Alisema, wahandisi chipukizi wanapomaliza masomo wamekuwa wakikaa muda mrefu bila kupata ajira hali inayosababisha wakate tamaa na kuichukia fani hiyo.

"Taasisi za serikali na zisizo za serikali tumieni wahandisi chipukizi, wapeni kazi za kihandisi ikiwa ni pamoja na kusajiliwa katika mfumo wa kufanya mazoezi ili kusaidia nchi kufikia uchumi wa viwanda," alisema.

Aidha, aliagiza Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB), kuhakikisha inawasilisha serikalini mapendekezo yaliyotolewa kwenye mkutano huo kama ilivyoelekezwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ili yatekelezwe. Pia aliiagiza bodi baada ya kuyawasilisha mapendekezo hayo serikalini, iyafuatilie, iwasiliane na vyombo husika ili kuhakikisha yanafanyiwa kazi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kadhalika, aliwapongeza wahandisi waliokula kiapo cha maadili ya utendaji kazi wao na kuwataka kuyaishi na kuyazingatia ili kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu za uhandisi.

"Wale wote ambao bado hawajala kiapo na wanajua wanapaswa kufanya hivyo, nawasihi wakafanye hivyo maana ni takwa la kisheria, ili kuwa na wahandisi wanaojua taratibu za fani hiyo na kukosa visingizio au kufanya makusudi kuharibu kazi kwa kisingizio cha kutojua taratibu hizo," alisisitiza.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Ninatubu Lema, alisema wanapendekeza kupitia mitaala ya elimu ya ngazi yote kwa lengo la kuiandaa nchi katika mapinduzi ya nne ya viwanda.

Pendekezo la pili, alilitaja ni kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kipekee na kuwa mkoa wa mfano na kuigawa.

"Kushawishi kupitia upya kwa sera, sheria na kanuni ili ziwe na tija na kufikia mapinduzi ya nne ya viwanda, hili ni pendekezo letu la tatu," alisema.

# Mafanikio 14 ya Jiji Dodoma kwa miaka 5

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetaja mafanikio 14 yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano kwenye elimu ya msingi ikiwamo uandikishaji wa darasa la kwanza umepanda kwa asilimia 121.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio ya halmashauri hiyo kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2019/20.

Alisema uandikishaji huo umepanda kutoka wanafunzi 13,277 ikiwa ni asilimia 101 ya lengo la uandikishaji mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 16,874 ambayo ni asilimia 121 ya lengo la uandikishaji kwa mwaka 2020.

"Kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli kumekuwapo na mabadiliko na mapinduzi makubwa katika maendeleo ya elimu ya msingi," alisema mkurugenzi huyo.

**Kutokana na hilo, ruzuku ya elimu bila malipo imeongezeka kutoka Sh. milioni 361.9 mwaka 2015/16 hadi Sh. milioni 918.2 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la Sh. milioni 556.2.**

Aidha, alisema kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa elimu ya awali kimeongezeka kutoka wanafunzi 9,214 ikiwa ni asilimia 114 ya lengo la mwaka 2015 hadi wanafunzi 10,939 ambayo ni asilimia 116 ya lengo la mwaka 2020.

Alibainisha kuwa mafanikio ya uandikishaji huo yametokana na mpango wa elimu bila malipo.

"Kutokana na hilo, ruzuku ya elimu bila malipo imeongezeka kutoka Sh. milioni 361.9 mwaka 2015/16 hadi Sh. milioni 918.2 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la Sh. milioni 556.2," alisema.

Pamoja na hayo alisema Jiji hilo limeongeza shule ya msingi hadi kufikia 141 zikiwamo 94 za serikali na 47 za binafsi, huku idadi ya watahiniwa kutoka 8,237 mwaka 2015 hadi 10,495 mwaka 2019 sawa na ongezeko la watahiniwa 2,258.

"Pia ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 62 mwaka 2015 hadi asilimia 85.36 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 23.36," alisema.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu, Mafuru alisema vyumba vya madarasa vimeongezeka kutoka 839 mwaka 2015/16 hadi madarasa 993 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 19.

"Matundu ya vyoo yameongezeka kutoka 1,028 mwaka 2015/16 hadi 1,223 mwaka 2019/20, nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 156 hadi kufikia 171," alisema.

Pia alisema madawati yameongezeka kutoka 11,115 hadi 15,291 kwa kipindi hicho sawa na ongezeko la asilimia 137.5.

"Jumla ya vitabu 298,785 vikiwamo vitabu vya darasani 252,107 na miongozo ya mwalimu 46,678 vimepokelewa na idadi hiyo imesaidia kuboresha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kutoka 1:7 hadi 1:3 kwa mwaka 2019/20," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri imejenga shule mpya ya



Mgombea ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, akizungumza na wananchi katika uzinduzi wa kampeni zake, viwanja vya Shule ya Msingi Chang'ombe, jijini Dodoma wikiendi. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# NHIF yaelezea kuongezeka kitita cha dawa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umesema kitita cha huduma za dawa kimeongezeka kutoka dawa 694 hadi 975.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema hakuna dawa iliyoondolewa kwenye kitita na kuwataka hofu wananchi kupuuza taarifa za mitandaoni.

"Kitita chetu kina jumla ya huduma 11 na yalifanyika maamuzi ya dhati ya kuongeza idadi ya dawa kwa kiasi kikubwa sana, kabla ya mwaka 2016 kulikuwa na mnyumbuliko wa dawa 694 lakini ziliongezeka na kufikia kwa sasa dawa 975, hili ni ongezeko kubwa," alisema.

Alisema kitita kina dawa zinazotosheleza ambazo Mtanzania atapata matibabu vizuri bila tatizo.

Aidha, aliwaagiza watoa huduma kuzingatia mikataba yao ya utoaji huduma kwa kutoa dawa kulingana na orodha ya dawa iliyopo kwenye kitita.

"Kumetokea sintofahamu kwa sababu kuna mtu alijitokeza kwenye taasisi yake na kuandika memo na kuanza kuisambaza kwenye mitandao, lakini mtoa huduma akumbuke ana mkataba na sisi azingatie mkataba na kama kuna tatizo lolote ni kati yetu na mtoa huduma," alisema.

Alisema taarifa inayosambaa inaonyesha orodha ya dawa zaidi ya 100 ambazo wanadai zimetolewa ikiwamo za magonjwa ya shinikizo la damu jambo ambalo si kweli kwa kuwa zote zipo kwenye mfumo.

Alieleza kuwa kuna mikataba ambayo wameingia na watoa huduma kwa kuambatanisha orodha ya dawa na huduma nyingi zinazotolewa.

"Kila baada ya miaka mitatu mikataba hiyo tumekuwa tukihuisha, tuna mfumo ambao wanatumia kuwasilisha madai, na kwenye mfumo tunazo dawa ambazo zimeorodheshwa na huduma nyinginezo," alisema.

Alisema mfuko umeanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kuweka madaktari wao kwenye hospitali ili kutoa ufafanuzi kwa watoa huduma na kwa wanachama.





# Shehena ya viuatilifu feki yanaswa Tunduma

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

TAASISI ya Utafiti wa Viuatilifu nchini (TPRI), imekamata shehena ya viuatilifu feki vya kuzuia wadudu waharibifu wa mazao zikiwa zimehifadhiwa na kuuzwa kwenye maduka mawili katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Viuatilifu hivyo vilikamatwa mwishoni mwa wiki wakati maofisa wa TPRI, maofisa wa Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) walipofanya ukaguzi wa kushtukiza katika mji huo, ambapo wafanyakazi watatu wa maduka hayo walitiwa nguvuni.

Mkaguzi na Mtafiti wa Viuatilifu wa TPRI kutoka Makao Makuu ya Taasisi hiyo jijini Arusha, Marciale Mkombozi, alisema walipata taarifa za siri kuwa kuna shehena ya viuatilifu hivyo vikiwa vimeingizwa katika mji huo na wakaamua kufanya ukaguzi ili kujiridhisha.

Alisema baada ya msako huo walibaini kuwa ni kweli kuna shehena hiyo ya viuatilifu ambavyo havikidhi ubora na viwango vya nchi na hivyo kuna uwezekano vikawa vina madhara kwa watumiaji.

**Viuatilifu hivi havijasajiliwa nchini na taasisi yenye dhamana hiyo ambayo ni TPRI, sasa hatujui ubora wake na hatujui madhara yake ni kiasi gani kwa watumiaji, kwa hiyo tunatakiwa kuviondoa kwa mujibu wa sheria.**

"Viuatilifu hivi havijasajiliwa nchini na taasisi yenye dhamana hiyo ambayo ni TPRI, sasa hatujui ubora wake na hatujui madhara yake ni kiasi gani kwa watumiaji, kwa hiyo tunatakiwa kuviondoa kwa mujibu wa sheria," alisema Mkombozi.

Vilevile, Mkombozi aliwataka wafanyabiashara wa viuatilifu kufanya kazi yao kwa kufuata sheria ili kuepuka kuchukuliwa hatua kali ambazo zinaelekezwa na sheria hizo ikiwamo kufungwa, kutozwa faini ama vyote viwili.

Mkaguzi wa viuatilifu kutoka TPRI Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mausa, aliwataka wananchi wanaotumia viuatilifu hivyo kuhakikisha wanavikagua kwanza ili kujua kama ni halali ama ni feki kwa kuangalia nembo ya usajili.

Alisema viuatilifu ambavyo watavibaini kuwa havina nembo ya TPRI havifai kutumika nchini na hivyo wanatakiwa kuachana navyo na badala yake watumie vilivyosajiliwa.

Alisema ili kuwarahisishia wananchi kutambua viuatilifu vilivyosajiliwa na ambavyo havijasajiliwa na TPRI, wameanzisha utaratibu maalumu wa kidigitali ambao mwananchi anakwangua namba maalumu na kuangalia.

"Tutawasambazia namba hizo kupitia kampuni ya TTCL, mwananchi akikwangua namba hizo na kuziingiza kwenye mtandao wetu wa TPRI, atabaini kuwa dawa anayotaka kununua imesajiliwa ama haijasajiliwa," alisema Mausa.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa maofisa wa taasisi hiyo ama kwa viongozi wa serikali ili hatua zichukuliwe mapema kabla viuatilifu hivyo havijasambaa maeneo mengine.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Tunduma Mjini, Edwin Nyilawila, alisema viongozi wa ngazi za chini za serikali wakiwamo wenyeviti wa mitaa wanaweza wakasaidia kudhibiti uuzwaji wa viuatilifu visivyoruhusiwa kutumika nchini.

Aliwaomba maofisa wa TPRI kutoa elimu kwa viongozi wa ngazi za chini ili wawe na uwezo wa kuvitambua viuatilifu ambavyo havijasajiliwa na vilivyosajiliwa ili wawe na uwezo wa kudhibiti.




Mwandishi wa Habari wa gazeti la Nipashe mkoani Mbeya, Grace Mwakalinga (kulia), akipokea cheti cha kuthamini mchango wa kampuni ya The Guardian Ltd kutoka kwa Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz, baada ya vyombo vya habari vya kampuni hiyo kuripoti kwa umahiri habari za kusaidia jamii mkoani Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mwang'ombe wa CHADEMA aahidi neema Mbarali

**Grace Mwakalinga,** MBARALI

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Liberatus Mwang'ombe, ameahidi kuboresha huduma za afya, elimu na mikopo kwa wanawake lengo ni kuhakikisha wanaishi kwa furaha na kutimiza malengo yao.

Mwang'ombe alitoa kauli hiyo, jana wakati akizungumza na Nipashe juu ya ahadi zake kwa wananchi kama atapata ridhaa ya kuwatumikia wana-Mbarali kama mbunge wao.

Alisema kiu yake ni kuona ajenda zinazohusu wanawake zinasimamiwa na kutekelezwa vizuri kwa kuhakikisha wanatengenezewa mazingira rafiki katika sekta ya afya, maji, elimu na mikopo.

"Kiu yangu ni kuona wana-Mbarali wanaishi maisha ya furaha na suala la kutengeneza furaha ni maamuzi yao, kwa kuhakikisha wanachagua kiongozi ambaye atakuwa karibu yao wakati wowote na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema Mwang'ombe.

Aliongeza kuwa atahakikisha huduma za mama na mtoto zinatolewa bure kwenye vituo vyote vya kutolea huduma, sambamba na uboreshaji wa mfumo katika utoaji mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Alisema kama sera ya CHADEMA inavyoelekeza kwamba utoaji wa huduma za afya kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano ataitekeleza kwa vitendo sambamba na kuhamasisha ujenzi wa hosteli kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike kusoma kwa utuliza na kutimiza ndoto zao.

Pia aliahidi kuyasaidia makundi maalum mikopo yenye masharti nafuu na mazingira bora ya upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

# Waunda jumuiya za maji kudhibiti uharibifu vyanzo

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

OFISI ya Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa imelazimika kuunda jumuiya za watumiaji wa maji ambazo zina katiba na sheria katika kuhakikisha vitendo vya uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji, mito na Ziwa Rukwa zinakomeshwa.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Maji Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Grace Chitanda, wakati akizungumzia jitihada zinazofanywa na ofisi hiyo katika kuhakikisha vyanzo vya mito na ziwa Rukwa vinahifadhiwa.

Alisema mbali na jitihada hizo, ofisi hiyo inaendelea na jitihada za kutunza vyanzo vya maji kati ya 16 na kati ya vyanzo hivyo vyanzo 8 vipo katika Jiji la Mbeya.

Alisema umefika wakati wananchi ni lazima wawe mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa wanavitunza vyanzo vya maji katika maeneo yao na si kusubiri mpaka serikali ichukue hatua, kwa kuwa vyanzo vya maji, mito na ziwa Rukwa ni muhimu katika maisha yao ya kila siku.

Grace aliitaja mito inayotiririsha maji katika Ziwa Rukwa ni Momba, Katuma, Songwe, Rungwa, Rwiche na Muze na kuwa mito hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kilimo kisichoziangatia utaalamu, hivyo kusababisha kiwango cha udongo unaoingia ndani ya ziwa hilo kuongezeka karibu kila mwaka.

"Mbali na jitihada zinazofanywa za kulinda na kulihifadhi mito na ziwa hilo bado kuna changamoto ya watu wengi kusababisha mito na Ziwa Rukwa kuendelea kujaa udongo kutokana na shughuli za ufugaji, uchimbaji wa madini na shughuli za kilimo hususani katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Mbeya, Rukwa na Songwe.

Alisema utafika wakati vyanzo vya maji na mito vikaishia kukauka iwapo jamii haitachukua hatua ya kukabiliana na uharibifu huo na kuwa ifahamike kuwa Ziwa Rukwa liliwahi kukauka kabisa na kupelekea baadhi ya viumbe ndani ya maji ya ziwa hilo kutoweka mwaka 1770.

Alisema mbali na Ziwa Rukwa kukauka ni wazi kuwa mwaka 1939 ziwa hilo lilijaa sana kwa mujibu wa kumbukumbu za miaka yote ya nyuma na kusababisha ongezeko la mvua mwaka huo.

Alisema umefika wakati ni lazima jamii ichukue hatua madhubuti za kuhakikisha vyanzo vya maji, mito na maziwa hayakauki kutokana na shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.





# NEC, asasi za elimu ya uraia wajadiliana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imekutana na asasi za kiraia ambazo zimepata kibali cha kutoa elimu ya mpigakura, ili kuisaidia jamii kupata elimu ya mpigakura na kutumia haki yao ya kidemokrasi ya kupiga kura kuchagua viongozi watakaofaa kuwaongoza.

Akifungua mkutano huo Visiwani Zanzibar Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura, Giveness Aswile, alizitaka taasisi hizo kujikita kwenye elimu ya mpiga kura na kuvitumia vibali walivyopewa kama ilivyokusudiwa na NEC.

Aliwataka wawakilishi wa asasi hizo kutochanganya elimu ya mpigakura na kampeni za vyama vya siasa na kutoegemea upande wowote katika utoaji wa elimu ya mpigakura.

Aidha, aliwataka kuwa makini na mambo ambayo yanaweza kuleta sintofahamu bila sababu yoyote ya msingi katika utoaji wa elimu hiyo.

**Kwa asasi ambazo zilibainika kufanya hivyo ni moja wapo ya sababu ya baadhi ya asasi hizo kukosa vibali v ya utoaji wa elimu ya mpigakura.**

"Mmepewa maelekezo ya kutotumia kwa ubia vibali mlivyopewa na Tume na asasi nyingine yoyote hasa zile ambazo hazijapata vibali," alisema.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa Tume inafahamu kuwa baadhi ya asasi zilizopewa vibali wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, zilitumia vibali vyao kwa ubia na asasi nyingine.

Alisema kwa asasi ambazo zilibainika kufanya hivyo ni moja wapo ya sababu ya baadhi ya asasi hizo kukosa vibali v ya utoaji wa elimu ya mpigakura.

"Tume inaendelea na itaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu, asasi yoyote itakayobainika kukiuka maagizo na maelekezo mliyopewa na Tume haitasita kusitisha kibali chake wakati wowote," alisema.

Hata hivyo, alieleza Tume katika elimu ya mpigakura haijaziachia asasi za kiraia na wadau wengine, bali pia inaendelea kutoa elimu kwa kutumia njia mbalimbali ili kuwafikia walengwa.

Naye Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina, alizitaka asasi hizo baada ya kutoa elimu hiyo kuhakikisha zinaharakisha ripoti kwa sababu baadhi ya asasi zimekuwa zikichelewesha kupeleka ripoti ZEC.

Aidha, aliwataka kuwa makini katika utoaji wa elimu ya mpigakura bila kuwakwaza ambao wanapaswa kupewa elimu ambao ni wapigakura.

Nao wawakilishi wa asasi hizo za kiraia walisema watafuata maelekezo waliyopewa na tume katika utoaji wa elimu, ili wananchi kutumia haki yao ya demokrasia ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Jumla ya asasi za kiraia 14 kutoka Zanzibar ziliomba kibali NEC kwa ajili ya utoaji wa elimu ya mpigakura, lakini asasi saba tu ndizo zilizopata kibali hicho baada ya kutimiza vigezo vinavyotakiwa na kuwa kwa Tanzania asasi 245 zimepata kibali kati ya 399 zilizoomba.




Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina, akizungumza katika kikao cha asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpigakura kwa ajili ya uchaguzi mkuu, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwinyi awafunda wagombea wa CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, amewataka wagombea wa uwakilishi, ubunge na udiwani wa chama hicho pamoja na wana CCM kushirikiana kuhakikisha wanapata ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza katika mkutano kati yake na wagombea wote wa CCM wa nafasi mbalimbali alisema uchaguzi wa kura za maoni katika chama hicho umemalizika na kilichombele yao sasa ni kushirikiana kwa pamoja ili kuhakikisha ushindi unapatikana.

Aliwataka wagombea hao kutoridhika kuomba kura katika majukwaa ya mikutano ya kampeni bali kwenda hadi kwa wananchi kuiombea kura CCM, ili ishinde.

Aidha, aliwataka aliwataka kufanya kampeni kwa kushuka katika ngazi za chini katika makundi mbalimbali wakiwamo waendesha bodaboda, mamalishe na makundi mengine ili kuwapigia kura wagombea wa CCM.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, aliwataka wagombea hao ambao wamepitishwa na chama na wasiopitishwa kutambua kuwa kuna kazi kubwa ya kuhakikisha CCM inashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Ninawapongeza wote waliojitokeza kuthubutu kugombea nafasi hizo na wapo ambao wamefanikiwa na ambao hawakufanikiwa, hivyo sote tunapaswa kushirikiana ili kuhakikisha CCM inashinda kwa kishindo," alisema.

Balozi Iddi aliwasihi wagombea ambao hawakupata nafasi katika uchaguzi wa mwaka huu kutonuna badala yake kushirikiana na wenzao katika kutafuta ushindi wa CCM.

Balozi Iddi aliwasisitiza wagombea hao kuhakikisha wanahubiri amani na usalama ambao ndio lulu ya taifa katika kuleta maendeleo.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdullah Juma Sadala 'Mabodi', alisema, ni jukumu la viongozi hao wakati wote kutangaza mafanikio ya ilani ya CCM na kuitangaza ilani mpya kwa mwaka 2020-2025 na kuhakikisha kuwa chama kinashinda kwa kishindo kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

## Waandishi watakiwa usawa kuripoti uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kutumia taaluma yao katika kuweka usawa wa kuandika taarifa za ukweli wakati wa kutangaza matokeo ya uchaguzi ili kuepuka uvunjifu wa amani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Vyombo vya Habari iliyoanzishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Mabruki Jabu Makame, kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha kamati hiyo kilichofanyika Zanzibar.

Alisema madhumuni ya kamati ya habari ni kuishauri ZEC katika kuendesha uchaguzi kupitia vyombo vya habari vya umma na binafsi katika hali ya usawa kwa vyama vyote vya siasa wakati wa kampeni.

Aidha, alieleza kuwa mwongozo huo unakusudia kutoa dira kwa vyama vya siasa vinavyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 vinapata nafasi ya kurusha hewani vipindi kuhusu sera na ilani zao kupitia vyombo vya habari vya serikali bila ya malipo.

Akichangia mada katika kikao hicho mjumbe wa kamati anayewakilisha chama cha ACT-Wazalendo, Salim Bimani, aliipongeza ZEC kwa kuandaa mwongozo mzuri na kuviomba vyombo vya habari kuvitekeleza kwa vitendo vifungu vya mwongozo huo.

Kwa upande wake Sheikhe Haji Dau kutoka ZEC na Mwinyi Mvua Nzukwi, Katibu wa Klabu ya Waandishi wa Habari waliwataka waandishi wa habari kufuata maadili ya taaluma ya uandishi wa habari wanaporipoti taarifa ili kuzuia mihemko ya kisiasa wakati wa baada ya uchaguzi.

Kamati ya vyombo vya habari iliyoanzishwa na ZEC kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu 2020 imeundwa na wawakilishi wa vyombo vya habari, taasisi za serikali na kutoka vyama vya siasa.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA, K**IWANJA CHA COMMERCIAL 1300SQM KINAUZWA KIPO REGENT ESTATE HAKUNA DALALI TUPIGIE: 0693 689996/ 0757 129546

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba ya gorofa moja inauzwa, ina frem 3 za biashara zote zinawapangaji. Ipo ukonga Dar es salaam. Simu 0757 07 90 57.

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FAITH BACKBORN CLINIC!!** TUNATIBU UTI WA MGONGO DISC PROBLEM KIUNO SELLULITIES GANZI PARALIZE BODY MEDICATED FULLBODY MASSAGE AND HOME SERVICES AVAILABLE 0714 919199

### NAFASI ZA KAZI

**TUNAHITAJI DEREVA WENYE SIFA ZIFUATAZO**

- UZOEFU USIOPUNGUA MIAKA 2
- UWEZO WA KUTUMIA EFD MASHINE
- UWEZO WA KUUZA MAJI YA CHUPA **SIMU: 0767 269677**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA VYETI



115889402

**KELVIN PETER FRANK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0534/0175** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. ANTHONY'S SEKONDARI mwaka 2010. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0167/0558** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIDUGALA LUTHERAN SEMINARY mwaka 2013. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/RUJ/RB/616634/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**RUFAA/MADAI NO 5/2020**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA.**

**SHAURI LA RUFAA JINAI NO. 165/1991**

**Katika mahakama ya mwanzo ya DODOMA MJINI**

**ANGELA P. MUSHI......................... Mrufani**

**DHIDI YA**

**SARA VARELIAN KANJE NA WENZAKE........................................Mrufaniwa**

**Kwa: DICKSON VARELIAN KANJE - DODOMA**

Kwa kuwa Rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya Jumatano Tarehe 9/9/2020 unatakiwa uhudhurie katika mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 19/08/2020.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA.

115889502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAMAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;261/2020**

**Ombi la ABRAHAM IGNATUS URASSA,Kuteu-liwa msimamizi wa mirathi marehemu PETER MELKIORY KIMARIO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 07/09/2020.

Tarehe 7/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115889602

---

### KUPOTEA KWA KADI

**Sanze Said Sanze** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki aina ya **TVS KING** yenye namba ya usajili **MC 864 CHV** iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania.Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo cha Polisi. Polisi taarifa: **RB/KAWE/2020**

115888002

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 202/2020**

**Ombi la MERY CHARLES POLE kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JOHN JOSEPH POLE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 02/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo ya JOHN JOSEPH POLE
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe ..........20.......

SAHIHI YA HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KAWE

215888702

---

### KUPOTEA KWA CHETI



115888602

**Abraham Shehe Kambi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne cehnye index namba **S0867-0051** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Pandahili. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **9910818512803**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;260/2020**

**Ombi la HARIETH SHABAN ABEID,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RUTHGARDAS PASCAL KAMAMKA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 15/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 07/09/2020.

Tarehe 7/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115889202

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ELIZABETH JOHN NDEORANO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 743 BXR** yenye chasis namba **GX1150001632** injini namba **1G6838339.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IR/TR/RB/1407/2020**

115889202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;259/2020**

**Ombi la REHEMA MOHAMED, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MWACHENI ALLY.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/09/2020.

Tarehe 4/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115889002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;237/2020**

**Ombi la SHABANI ALLY MAKUSI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AWADHI MAKUSI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/08/2020.

Sahihi ya Hakimu

115888902

---

### KUPOTEA KWA CHETI



115888102

**JUMA M. HATIBU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3037-0152** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NYAMAGANA SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No: **9910818968117.**

---

**TANGAZO LA KUITWA MAHAKAMANI**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**SHAURI LA MAOMBI NAMBA 161 YA MWAKA 2003**

**EDWARD KILANGA.......................MUOMBAJI.**

**DHIDI YA**

**ATHONIA ZACHARIA..............MUJIBU MAOMBI.**

**KWA; ATHONIA ZACHARIA**
**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba muombaji amefungua shauri la maombi ya kukaza hukumu dhidi yako na nakala yake inapatikana katika Mahakama hii.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 23/09/2020 saa 2;30 asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya maombi haya.
Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa Mahakama hii leo tarehe **01/09/2020.**

HAKIMU MKAZI MWANZA

115889302

---


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Saudia yasisitiza kujitosa suluhisho kwa Wapalestina

**RIYADH, Saudi Arabia**

MFALME Salman wa Saudi Arabia, amesema anaunga mkono suluhisho la usawa litakalowazingatia Wapalestina.

Msimamo wa mfalme huyo wa Saudi Arabia aliutoa katika mazungumzo yake ya simu na Rais wa Marekani, Donald Trump, wakati akiusifu ufalme huo kwa hatua yake ya kufungua anga yake kuruhusu ndege za Israel zinazotokea Umoja wa Falme za Kiarabu UAE kuingia katika anga lake.

Saudi Arabia ilisema haitofuata msimamo uliochukuliwa na Umoja wa Falme za Kiarabu, uliotangaza mwezi uliopita kwamba utaanzisha uhusiano wa kidiplomasia na Israel, hadi pale dola ya Wayahudi litakaposaini makubaliano ya amani na Wapalestina yanayotambuliwa kimataifa.

Wiki iliyopita Saudi Arabia ilikubali kuruhusu safari za ndege zote kutoka UAE kupita kwenye anga lake wakati ambao Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, akitangaza kuanzisha safari za moja kwa moja kutoka Tel Aviv Israel hadi Abu Dhabi.

*DW*



Maofisa wa afya wakiendelea kutoa huduma dhidi ya corona kwa wananchi nchini India. **PICHA: DW**

# India ya pili visa vingi COVID-19

**NEW DEHLI, India**

INDIA imeipiku Brazil na kuwa ya pili yenye idadi ya kubwa ya visa vya virusi vya corona na kuwa nyuma ya Marekani, huku ikiwa imevifungua vituo vyake vya treni vilivyofungwa kwa takriban miezi sita.

Kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha Johns Hopkins, katika kipindi cha saa 24, India imerekodi visa vipya 90,802 na hivyo kuifanya nchi hiyo kuwa na visa milioni 4.2 ikiwa nyuma ya Marekani yenye visa milioni 6.2.

Siku ya Jumatatu Wizara ya Afya ya India pia ilirekodi vifo vipya 1,016 na kufanya jumla ya watu waliokufa kutokana na ugonjwa wa COVID-19 kufikia 71,642, ikiwa nchi ya tatu duniani yenye vifo vingi.

Katika wiki za hivi karibuni, India ambayo ni ya pili duniani kwa kuwa na watu wengi wanaofikia bilioni 1.4, imekuwa eneo jipya lenye visa vingi vya virusi vya corona, ingawa visa vinaendelea kuongezeka ulimwenguni kote ambako kuna wagonjwa takriban milioni 27 na zaidi ya vifo 880,000.

Ufaransa, Israel na Australia ni miongoni mwa nchi zilizolazimika katika siku za hivi karibuni kuongeza vizuizi vya usafiri au kuweka vingine vipya katika juhudi za kudhibiti maambukizi mapya.

*DW*

# 20 wauawa mapigano Yemen

**SANA'A, Yemen**

ZAIDI ya watu 20 wameuawa katika mapigano mkoa wa Kaskazini mwa Yemen wa Al Jawf wakati wanajeshi wa serikali walipojaribu kuyakomboa maeneo yao waliyoyapoteza kwa waasi wa Kihouthi miezi kadhaa iliyopita.

Serikali ya Yemen inayotambuliwa kimataifa imekuwa ikipambana na waasi hao wanaoungwa mkono na Iran tangu mwaka 2014, baada ya waasi hao kuidhibiti sehemu kubwa ya Kaskazini ikiwamo Mji Mkuu Sanaa.

Katika mapambano ya juzi, taarifa za Jeshi la Serikali zimeeleza kwamba Wahouthi 16 na wafuasi wake wanane waliuawa.

Chanzo kilichotoa taarifa hiyo kwa shirika la habari la AFP kimefahamisha kwamba wanajeshi wa serikali waliwakamata waasi zaidi ya 40. Wakati huo huo wana mgambo walisogea hadi kwenye mji jirani wa Marib katika Wilaya ya Mahliya baada ya kutokea mapigano makali ambayo yalisababisha umwagikaji damu.

*DW*

## Waandamanaji 633 wakamatwa Belarus

**MINSK, Belarus**

JESHI la Polisi nchini Belarus, limewakamata watu 633 katika maandamano yaliyofanyika nchi nzima juzi Jumapili.

Taarifa hiyo ilitolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani kuwa, maofisa walianzisha hatua ya kuwaandaa waandamanaji kumpinga Rais Alexender Lukashenko, maandamano yaliyozuka baada ya uchaguzi wa Agosti 9, mwaka huu, unaotajwa na wapinzani wake kwamba uligubikwa na udanganyifu.

Wakati huo huo katika taarifa iliyotolewa na Ikulu ya Urusi jana, ilieleza kuwa, kiongozi huyo wa Belarus atakwenda nchini Urusi siku chache zijazo kwa ajili ya mazungumzo na serikali mjini Moscow. Taarifa hiyo imetolewa na ikulu ya Urusi leo.

**DW**

## Achoma nyumba akiua nzi

**PARIS, Ufaransa**

MWANAUME mwenye umri zaidi ya miaka 80, amechoma nyumba yake iliyoko kando ya mto Dordogne nchini Ufaransa, wakati akijaribu kuua nzi aliyekuwa akimzunguka.

Mzee huyo, aliamua kuchukua kifaa cha umeme kilichotengenezwa kwa ajili ya kuwaua mende akaanza kumuua nzi huyo, lakini kwa bahati mbaya gesi ilikuwa inavuja katika nyumba.

Gesi na kifaa chake vilisababisha mlipuko na sehemu ya paa la nyumba yake iliyopo katika Kijiji cha Parcoul-Chenaud ikaharibika.

Kulingana na taarifa za vyombo vya habari nchini humo, mwanaume huyo ambaye hakuwa na silaha alibahatika kutoroka akiwa ameungua tu kwenye mkono wake.

Chombo cha Habari cha Sud-guest, kilisema kuwa hatima ya nzi huyo bado haijajulikana.

Mwanaume huyo kwa sasa amejihifadhi katika hoteli moja ya eneo hilo huku familia yake ikikarabati nyumba yake.

**BBC**

**Mzee huyo, aliamua kuchukua kifaa cha umeme kilichotengenezwa kwa ajili ya kuwaua mende akaanza kumuua nzi huyo, lakini kwa bahati mbaya gesi ilikuwa inavuja katika nyumba.**

HABARI MICHEZO




# FATI AWEKA REKODI MPYA KIKOSI CHA HISPANIA

**MADRID, Hispania**

ANSU Fati amekuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mdogo zaidi kufungia Hispania bao kwenye historia ya timu hiyo ya taifa, wakati wa mchezo dhidi ya Ukraine, Jumapili.

Fowadi huyo wa klabu ya Barcelona alicheza mchezo wake huo wa kwanza kwa Hispania wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye dimba la Alfredo Di Stefano.

Akiwa na umri wa miaka 17 na siku 311, Fati amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuifungia Hispania.

Ulikuwa ni mwanzo mzuri zaidi kwa Fati, ambaye alizawadiwa penalti iliyofungwa na Sergio Ramos ambaye ndiyo alifunga bao la uongozi, kabla ya yeye kuongeza la pili.

Fati alianza kuwapo kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Hispania wakati alipowekwa benchi kwenye sare ya bao 1-1 na Ujerumani, mchezo uliopigwa Alhamisi iliyopita.




## Ancelotti asifia usajili wa Allan

**LONDON, England**

NYOTA mpya aliyesajiliwa na Everton, Allan ni mmoja wa viungo bora wakabaji duniani, kwa mujibu wa bosi wa Toffees, Carlo Ancelotti.

Everton ilithibitisha kumsajili Allan kutoka Napoli Jumamosi, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 akisaini mkataba wa miaka mitatu ya kukaa hapo Goodison Park.

Allan alikuwa mmoja wa wachezaji wenye kipaji cha juu kwa kikosi hicho cha Serie A chini ya makocha, Maurizio Sarri na Ancelotti, lakini hakuwa chaguo la kocha, Gennaro Gattuso.

Ancelotti ameamua kuuungana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil - ambaye amecheza mechi tisa kwa nchi yake na amesajiliwa Everton kwa ada iliyoripotiwa euro milioni 22.2.

Huku dili kwa nyota wa Real Madrid, James Rodriguez na mkali wa Watford, Abdoulaye Doucoure zikionekana kukaribia, Ancelotti amemsifia Allan, ambaye alishuhudia timu yake mpya ikiifunga Preston North End mabao 2-0 kwenye mechi ya kirafiki Jumamosi, kuwa ni mmoja wa wachezaji bora kwenye kikosi chake.

"Nina furaha kwa hili," amesema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

## Roma yaingia vitani na Barcelona kwa Depay

**ROME, Italia**


NYOTA anayewaniwa na Barcelona, Memphis Depay pia anawindwa na AS Roma, rais wa Lyon, Jean-Michel Aulas amebainisha.

Nahodha huyo wa Lyon, Depay yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake na miamba hao wa Ligue 1 na amekuwa akihusishwa na uhamisho wa fedha nyingi kwenda Barca.

Fowadi huyo wa zamani wa Manchester United awali alifanya kazi na kocha mpya wa sasa wa Blaugrana hao, Ronald Koeman akiwa na kikosi cha Uholanzi.

Lakini Aulas ameonya kwamba dili na Barca bado halijafanyika wakati akielezea nia hiyo ya AS Roma kwa mchezaji huyo.

Aliiambia Telefoot: "Mkataba wa Memphis unamalizika. Koeman anamtaka yeye kule Barcelona, lakini Roma wanamtaka




mchezaji huyo."

Depay amerudi uwanjani baada ya kuumia akiiongoza Lyon kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, awali akiwa amewafunga mabao tisa kwenye mechi 13 za Ligue 1 msimu uliopita.

Wiki iliyopita alifunga hat-trick kwenye mchezo wa kwanza wa Lyon kwenye Ligue 1 msimu huu wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Dijon.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alijiunga na Lyon kutoka United kwa euro milioni 16 mwaka 2017 na sasa ameripotiwa kuwa thamani yake ni euro milioni 25.

## HABARI MICHEZO



# HATIMA YA MARTINEZ KUJULIKANA WIKI HII

**BARCELONA, Hispania**

NAFASI ya Barcelona kumsajili nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez inaweza kuwekwa wazi wiki hii, kwa mujibu wa gazeti la Sport.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, bado ina nia ya kutaka kumsajili fowadi huyo wa kimataifa wa Argentina, ambaye alifunga mabao 21 kwa Inter msimu wa 2019-20.

Sasa dili hilo linaweza kufanikishwa mapema wiki hii na kila kitu kitajulikana na kuwa wazi.

Wakala wa Martinez atakutana na viongozi wa Inter wiki hii kujadiliana nao ili kufikia muafaka kuhusu majaliwa ya mteja wake huyo.

Ripoti zinasema kwamba, Barcelona na Inter wamekuwa wakiwasiliana mara kwa mara, lakini kuna tofauti kubwa kati ya klabu hizo mbili kwenye makubaliano ya kiasi cha fedha.

Imesemwa kwamba, Barca wanataka kulipa kiasi cha juu cha euro milioni 65 kwa ajili ya mchezaji huyo, wakati Inter Milan wanataka angalau kiasi cha euro milioni 85.

Goal.com imeripoti kwamba Barcelona wanaandaa ofa yao ya mwisho kwa Martinez.

## SANCHO AZUNGUMZIA THAMANI YAKE

**DORTMUND, Ujerumani**

JADON Sancho amebakia kuwa mnyenyekevu kwa bei iliyowekwa na Borussia Dortmund kwa mauzo yake huku kukiwa na ripoti ya kuwaniwa na Manchester United.

Hata hivyo, nyota huyo wa England ametaka utulivu kuhusu uvumi huo na majaliwa yake ya baadaye.

United imekuwa ikihusishwa sana na uhamisho wa Sancho, ingawa Dortmund imerudia kusisitiza hawatamuuza mchezaji huyo kuelekea msimu huu wa 2020-21.

Sancho amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji bora vijana barani Ulaya msimu uliopita baada ya kufunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho 16 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wakati Dortmund ikimaliza nafasi ya pili, na hivyo timu kama Real Madrid, Liverpool na Barcelona kuibuka kumwania.

Miamba wa Ligi Kuu ya England, United wameripotiwa kuendelea kujaribu kufanya makubaliano na Dortmund - ambao bado hawajaondoa kipengele cha thamani ya mchezaji huyo ya pauni milioni 108.

"Lakini kwa upande wangu tena, siangalia kiasi hicho. Kwa upande wangu ni suala la kufanya vizuri kwa timu na mimi mwenyewe."

# Low: Ujerumani bado haipo sawa

**BASLE, Uswisi**

JOACHIM Low anahisi kikosi chake cha Ujerumani hakipo vizuri kwa ajili ya mashindano baada ya kutoka sare ya pili ya kufungana 1-1 na Uswisi kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Ujerumani bado inasubiria ushindi wake wa kwanza kwenye ligi hiyo baada ya pia kutoka sare ya kufungana bao 1-1 na Hispania.

Ilkay Gundogan aliipa bao la uongozi Ujerumani dakika ya 14, lakini walikosa nafasi nyingi za wazi za kufunga, kabla ya Silvan Widmer kusawazisha kipindi cha pili.

Ujerumani imepitwa pointi mbili na Hispania kwenye kundi lake la A4 na kocha mkuu Low anahisi kuwakosa wachezaji kadhaa kutoka kikosi cha Bayern Munich kilishoshinda mataji matatu, kumewafanya washindwe kuwa kwenye ubora wao.

"Kama ilivyokuwa dhidi ya Hispania, tulishindwa kufunga bao kipindi cha pili, kitu ambacho kingetupa sisi ulinzi," alisema akiiambia ZDF.

"Mara mbili mfululizo tumeanza kwa kuongoza kwa 1-0, na mara mbili tumeshindwa kurudi nyumbani na kitu chochote. Tulikuwa na nafasi nzuri, lakini tuliwaacha Uswisi warudi mchezoni kipindi cha pili.

"Tulipoteza mipira mingi, na sare hiyo ni kama hatukustahili. Baadhi ya wachezaji hawakuwa kwenye ubora wao kwa ajili ya mashindano, wachezaji wengine hawakuwapo kabisa."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI NUSURA ASAJILIWE PSG

●●●Wakati tulipoambiwa Messi anataka kuondoka, tulishawishika kutaka kumsajili, lakini...

**PARIS, Ufaransa**

MKURUGENZI wa michezo wa Paris Saint-Germain, Leonardo, amebainisha kwamba mabingwa hao wa Ligue 1 walishawishika kumsajili nyota wa Barcelona, Lionel Messi, huku akisisitiza Neymar na Kylian Mbappe lazima wabakie klabuni hapo.

Messi awali aliwasilisha maombi ya kutaka kundoka, lakini nahodha huyo wa Barca na mshindi mara sita wa Ballon d'Or atabakia pale Camp Nou kwa msimu wa 2020-21.

Manchester City walikuwa wakihusishwa zaidi na usajili wa Messi, huku PSG pia walikuwa tayari kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33.

"Leo hii ukifikiria kuhusu masuala ya kifedha, ni magumu," amesema Leonardo akiiambia Canal+ wakati alipoulizwa kama PSG walikuwa na nia ya kumsajili.

"Wakati tulipoambiwa kwamba Messi anataka kuondoka, tulishawishika kutaka kumsajili. Lakini tulikuwa tunajiambia wenyewe itawezekana? Maana wachezaji wengine ni ngumu kufanya nao majadiliano.

"Sijui, David Beckham hatimaye alikuja Paris Saint-Germain, Messi atakuja Paris? Sijui.

"Ni mambo ya soka, mwisho wa siku kila mmoja atakaa mezani, kila mmoja anajua kila kitu kwamba mambo yanakwenda mbele."

Kumekuwa pia na uvumi kuhusu wakali wawili wa PSG, Neymar na Mbappe kuwa njiani kuondoka klabuni hapo baada ya kupoteza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu yake ya zamani ya Barca, huku pia Real Madrid haijaficha hisia zake za kutaka kumsajili Mbappe.

Hata hivyo, Leonardo amesema: "Tunataka kuendelea kuwa nao. Kila kitu kipo wazi kwa kila mmoja. Lazima tuendelee kuwa nao."

## KWA UFUPI

**FRASER ATUA RASMI NEWCASTLE**
WINGA wa Scotland, Ryan Fraser mwenye umri wa miaka 26, amekubali kujiunga na Newcastle United baada ya kuondoka Bournemouth na jana Jumatatu alifanyiwa vipimo vya afya. ***(Sky Sports)***

**OLE AZUNGUMZA NA SANCHO**
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amezungumza na winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, kuhusu kujiunga na klabu hiyo kutoka Borussia Dortmund kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Express)***

**BADO HAKUNA OFA YA BALE**
LICHA ya Gareth Bale kutaka kuondoka Real Madrid, klabu hiyo bado haijapokea ofa yoyote kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales. ***(Mundo Deportivo)***

**KOEMAN KUMBAKIZA COUTINHO**
KOCHA mpya wa Barcelona, Ronald Koeman, ameiambia klabu hiyo anataka kumbakiza Philippe Coutinho msimu huu kuliko kumpeleka kwa mkopo sehemu nyingine nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 28. ***(Marca)***

**SUAREZ SAFARI IMEIVA JUVE**
FOWADI wa Barca, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 33, jana Jumatatu alitarajia kuanza mazoezi ya lugha, ili kupata uraia wa Italia, na kuweza kuruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay kukamilisha uhamisho wake kwenda Juventus. ***(Eurosport)***

**REAL MADRID KUKIFUMUA KIKOSI**
REAL Madrid inapanga kukifanyia mabadiliko makubwa kikosi chake kwa kiasi pauni cha milioni 261 na wanataka kumsajili nyota wa Borussia Dortmund raia wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 20, na straika wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21. ***(ABC Spain)***

**DEPAY AWANIWA ROMA**
KLABU ya AS Roma imeungana kwenye mbio moja za kutaka kumsajili fowadi wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 26. ***(Goal)***

**GIANLUIGI ATAKA MKATABA MPYA MILAN**
GOLIKIPA wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 21, anataka mkataba mpya wenye thamani ya euro milioni 10 kwa msimu, wakati akiwa anawaniwa na Chelsea. ***(Corriere della Sera, via 90min)***

**LEICESTER YAKATAA BEI YA WESLEY**
LEICESTER City haipo tayari kulipa pauni milioni 27 kwa Saint-Etienne ili kumsajili mlinzi wake, Wesley Fofana, lakini wapo tayari kufikia makubaliano ya kutoa pauni milioni 18 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ufaransa. ***(Mail)***

**DZEKO AOMBA KUONDOKA ROMA**
STRAIKA wa Bosnia-Herzegovina, Edin Dzeko mwenye umri wa miaka 34, ameomba kuondoka AS Roma ili ajiunge na Juventus. ***(Corriere dello Sport)***

**BARCA OFA YA MWISHO KWA MARTINEZ**
BARCELONA inaandaa ofa ya mwisho kwa straika wa Inter Milan raia wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 23. ***(Goal)***



HABARI MICHEZO

# MISIMU 13 SASA SIMBA SC HAIJAFUNGWA UFUNGUZI

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-1 ilioupata Simba Jumapili iliyopita dhidi ya Ihefu FC kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, umeifanya timu hiyo kucheza misimu 13 ya Ligi Kuu bila kupoteza mechi yoyote ile ya ufunguzi.

Yalikuwa ni mabao ya John Bocco na Mzamiru Yassin, yaliyotosha kuendeleza rekodi yao safi linapokuja suala la mechi za mwanzo wa ligi.

Mara ya mwisho Simba kupoteza mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu ilikuwa ni 2007/08, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga.

Ilikuwa ni Septemba 23, kwa bao pekee lililofungwa na Sunday Peter.

Baada ya hapo Simba imecheza kwa misimu yote 13, ikishinda mechi 11 za mwanzo wa msimu na kutoa sare mbili tu.

Rekodi zinaonyesha kuwa mechi zote hizo 13 ambazo Simba imecheza, sita ilicheza ugenini na saba ilianzia nyumbani, huku sare ambazo ilizopata moja ilikuwa nyumbani na nyingine ugenini.

Msimu wa 2008/09, iliichakaza Villa Squad mabao 4-1, kabla ya kuichapa Majimaji mabao 2-0 2009/10, na ikashinda mabao 2-0 dhidi ya African Lyon msimu wa 2010/11. Simba iliendeleza rekodi yake safi msimu wa 2011/12 ilipoifunga JKT Oljoro mabao 2-0, na African Lyon mabao 3-0 msimu wa 2012/13, kabla ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 ugenini dhidi ya Rhino ya Tabora mechi ya ufunguzi msimu wa 2013/14.

Sare nyingine ya mabao 2-2 ilipatikana msimu wa 2014/15, ilipocheza dhidi ya Coastal Union, huku 2015/16 ikishinda bao 1-0 dhidi ya African Lyon, kabla ya kushinda mabao 3-1 msimu wa 2016/17 ilipoanza na Ndanda FC.

Ilipa kipigo cha mabao 7-0 Ruvu Shooting msimu wa 2017/18, ikaifunga Prisons bao 1-0 msimu wa 2018/19, ikaiadhibu JKT Tanzania mabao 3-1, 2019/20, na Jumapili iliyopita msimu wa 2020/21 ilianza pia kwa ushindi wa mabao 2-1.



Baadhi ya wanariadha wa mbio za Serengeti Migration Marathon, wakishiriki mbio hizo, zilizodhaminiwa na kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), pamoja na kampuni nyingine kwa ajili ya uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira, zilizofanyika wilayani Serengeti, mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Biashara afurahia ushindi wa kwanza

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Biashara United, Francis Baraza, amesema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo wa Ligi Kuu, baada ya kuifunga Gwambina FC bao 1-0.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka mkoani Mara, Kocha huyo alisema amefurahi kupata pointi tatu licha ya mchezo kuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa.

"Nawapongeza wachezaji wangu wamefanya kazi kubwa, wamefuata maelekezo ambayo niliwapa na yamewasaidia kupata pointi zote tatu," alisema Baraza.

Alisema waliingia kwenye mchezo huo wa tahadhari kubwa kutokana na kuwa walicheza na timu ambayo ni ngeni kwenye Ligi Kuu.

Alisema wachezaji wake walitumia dakika 45 kuwasoma wachezaji wa timu ya Gwambina, na wakafanikiwa kupata ushindi huo.

"Tuliwasoma muda mrefu, wachezaji wangu walipowajua wakaweza kupata ushindi mzuri dakika za lala salama na ninaahidi kufanya vizuri kwenye mechi zinazofuata."

Alisema katika mchezo huo aliathirika kwa kiasi kikubwa baada ya kushindwa kuwatumia nyota wake saba wa kigeni, kutokana na vibali vyao vya kazi kuchelewa kufika.

## Mafunzo kutema wachezaji wanane

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Mafunzo inatarajia kuwatema wachezaji wanane katika msimu huu wa usajili kuelekea msimu mpya wa 2020-21, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Mafunzo, Makame Fadau, alisema sababu kubwa ya kuachana na wachezaji hao ni kutona na kushuka viwango vyao na wengine umri wao kubwa mkubwa.

Alisema wachezaji hao anaowaacha kati yao ni kutoka kikosi cha kwanza cha timu hiyo kwa msimu wa ligi iliyoisha 2019-20, ingawa hakuweka wazi majina ya wachezaji hao akidai ni mapema mno kwa sasa kuwataja.

"Tunaachana na wachezaji wanane, ili kutoa fursa kwa timu kusajili kikosi kitakacholeta mafanikio zaidi na wapo baadhi ya wachezaji pia tutawatoa kwa mkopo kwa msimu huu," alisema Fadau.

Aidha, alisema timu hiyo kwa hivi sasa imejipanga kuhakikisha inafanya vizuri kwa kusajili wachezaji vijana na wenye uwezo wa kucheza mpira utakaoleta ushindani katika Ligi Kuu.

Hata hivyo, alisema timu hiyo kwa msimu huu inataka kusajili wachezaji watakaowawezesha kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar kwa msimu wa 2020-21.

## Kikao cha Wahenga kuonekana videoni

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kufanikisha uzinduzi wa albamu mpya ya 'Kikao cha Wahenga', bendi ya muziki wa dansi ya Waluguru Original, imesema, kinachofuata sasa ni kushuti video ya baadhi ya nyimbo za albamu hiyo.

Mkurugenzi wa bendi hiyo yenye maskani yake mjini Morogoro, Killer Man, aliliambia gazeti hili kuwa kazi ya kushuti video itafanyika kwenye maeneo mbalimbali ya mji huo, wiki mbili zijazo.

"Albamu yetu ya 'Kikao cha Wahenga ina nyimbo za Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe', lakini tutaanza na nne," alisema Killer Man.


Alisema, walizindua albamu mwanzoni mwa mwezi uliopita na kufanikiwa kujizolea mashabiki wengi, na kwamba tangu wakati huo, mashabiki wanaulizia video ya nyimbo za albamu hiyo.

"Uzinduzi wa albamu yetu ulikuwa ni moja ya mikakati yangu ya kutaka kurudisha shamrashamra za muziki wa dansi katika mji wa Morogoro, ambazo zilianza kupotea mwishoni mwa miaka ya sabini," alisema.

Killer Man alisema, mji wa Morogoro ulitamba katika dansi ukiwa na wanamuziki maarufu wengi kama Mbaraka Mwishehe na wengine, lakini baadaye mambo yalibadilika, sasa anarudisha hali hiyo taratibu.

Alifafanua kuwa, bendi yake ilianza kazi mwaka 2014 ikiwa na albamu iliyopewa jina la 'Rosemary ', na sasa imekuja na 'Kikao cha Wahenga', ambayo alidai ni imechangia kuipa umaarufu bendi hiyo.

Michezo
Jumanne Septemba 8, 2020
Nipashe



MESSI NUSURA ASAJILIWE PSG

HABARI UK 22




Ansu Fati akiifungia bao Hispania kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Ukraine mjini Madrid. Hispania ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# SVEN AKIRI MUZIKI WA IHEFU NI BALAA

●●●Airudisha Simba mapema Dar kujiandaa kuifuata Mtibwa, asema huu ni mwanzo lakini....

**Na Isaac Kijoti, MBEYA**

LICHA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu jana, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema haikuwa kazi rahisi.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa, pamoja na Simba kumiliki mpira, lakini Ihefu iliionyesha upinzani mkali kwa dakika zote 90.

Kilichoiangamiza Ihefu ni uzoefu mkubwa wa wachezaji wa Simba na uwezo binafsi wa mchezaji mmoja mmoja.

Shukrani ya ushindi huo ni kwa nahodha John Bocco aliyeanza kuliona lango dakika ya 10 na Yassin Mzamiru dakika ya 42, huku la Ihefu likizamishwa nyavuni na Omar Mponda dakika ya 14.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Sven alisema alijua hata kabla ya mchezo huo na kabla ya kushuka dimbani aliwatahadharisha wachezaji wake kuwa mechi itakuwa ngumu.

> **"Nilijua mechi itakuwa ngumu kwa sababu Ihefu ndiyo kwanza inacheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza itataka kuonyesha uwezo wake na wamefanya hivyo kwa kutoa upinzani mkubwa kwetu.**

"Kikubwa tumepata ushindi na hii ni mechi ya kwanza, tutaendelea kujiimarika kwa michezo ijayo," alisema Sven.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Maka Mwalusi, aliipongeza timu yake kwa kuweza kutoa ushindani dhidi ya timu kubwa kama Simba, ambayo ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo.

"Kwanza niliwaambia wachezaji wangu wacheze kwa kuwaheshimu Simba, lakini kwa kufanya mashambulizi ya kushtukiza.

"Kwa hilo tulifanikiwa na kuonyesha mchezo mzuri, hivyo kama tumeweza kuonyesha uwezo mkubwa kwa timu kama Simba, naamini mechi zijazo tutafanya vizuri zaidi," alisema Mwalusi.

Simba iliondoka jana asubuhi jijini hapa kurejea Dar es Salaam kujiandaa kuifuata Mtibwa Jumamosi.

## ZLATKO: WAZAWA YANGA SC HAWAWEZI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukiongoza kikosi chake kwa mara ya kwanza na kushuhudia kikilazimishwa sare ya bao 1-1, dhidi ya Tanzania Prisons, Kocha Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema tatizo ni pumzi kwa wachezaji wazawa.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Zlatko aliwaanzisha wachezaji wote wazawa isipokuwa mshambuliaji wa kati tu, Mghana Michael Sarpong.

Hadi timu hizo zinakwenda mapumziko zilifungana bao 1-1, Prisons ndiyo ilikuwa ya kwanza kupata bao kupitia kwa Lambart Charles, huku Sarpong akiisawazishia Yanga.

Kipindi cha pili, Zlatko alifanya mabadiliko makubwa kwa kuwaingiza Wakongomani Tuisila Kisinda na Mukoko Tunombe pamoja na straika raia wa Burkina Faso, Sogne Yacouba.

Lakini akizungumza baada ya mchezo huo, Zlatko alisema amebaini wachezaji wa Tanzania katika kikosi hicho hawana pumzi ya kuweza kucheza kwa dakika zote 90.

"Wachezaji wa Tanzania hawakuwa fiti kuweza kucheza kwa dakika zote 90, hata hawa wageni walielezwa programu ya mchezo muda mfupi kabla ya mechi," alisema Zlatko.

Hata hivyo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, aliitetea kauli hiyo ya bosi wake akieleza alimaanisha kwamba alikuwa na muda mfupi wa kusoma uwezo wa mchezaji mmoja mmoja.

"Hakuwa na maana hiyo, alimaanisha bado hajapata muda wa kutosha kumsoma mchezaji mmoja mmoja na si kuhusu 'fitness' ya wachezaji wazawa," Mwambusi alifafanua.

Kikosi cha Yanga kinaundwa na wachezaji wengi wapya ikiwa ni pamoja na benchi jipya la ufundi, jambo ambalo Zlatko tangu awali alishasema anahitaji muda kukisuka.

Aidha, Zlatiko alisema baada ya matokeo hayo wanaenda kufanyia kazi upungufu uliyojitokeza katika mchezo uliopita na sasa wanahitaji kufanya vizuri na kuondoka na pointi tatu muhimu dhidi ya Mbeya City.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >